# Nipashe

Jumamosi Mei 18, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579921

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




Simulizi mume alivyookolewa na samaki kuzama baharini

UKURASA 3







UKURASA 13

# URAIS 2020 Kazi imeanza

UKURASA 2



Membe Rostam

# Aliyemgomea Ndugai aibua mambo mazito

**AMTWISHA** zigo la tuhuma bosi wake, Mbunge Msigwa amshangaa Spika... *Endelea Ukurasa. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MGODI ACACIA WATOZWA FAINI YA BILIONI. 5.6/-**

SERIKALI imeutoza faini ya Sh. bilioni 5.6 mgodi wa dhahabu wa North Mara (Acacia) ulioko Tarime mkoani Mara...

UKURASA WA 3

**JPM ATENGUA UTEUZI WA WAKURUGENZI WAWILI**

RAIS John Magufuli, ametengua uteuzi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi Mkoani Songwe, Adelius Makwega...

UKURASA WA 4

**BANDARI YA BAGOMOYO SERIKALI INAENDELEA NA MAJADILIANO YA UJENZI**

SERIKALI imesema inaendelea na majadiliano ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo iliyopo Mkoa wa Pwani ili kuangalia kama kiuchumi itakuwa na tija kwa Tanzania na endapo...

## Mambo 9 yatajwa kupaisha kilimo

UKURASA 3

**HABARI** HOTUBA KAMILI WIZARA YA KILIMO UK. 25

MAONI, KATUNI UK.6

## Mgodi acacia watozwa faini bil. 5.6/-

**Na Anthony Gervas,** TARIME

SERIKALI imeutoza faini ya Sh. bilioni 5.6 mgodi wa dhahabu wa North Mara (Acacia) ulioko Tarime mkoani Mara, baada ya kushindwa kujenga bwawa jipya la kuhifadhi maji machafu yenye sumu, hivyo kuendelea kutiririsha na kuingia kwenye makazi ya watu.

Kampuni hiyo ilitozwa faini hiyo juzi na mawaziri wa Madini, Doto Biteko, na wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), Januari Makamba walipofanya ziara ya kushtukiza mgodini hapo.

"Tangu wananchi waanze kulalamikia maji haya kuwa ni machafu yana sumu, leo ni miaka 10 sasa tangu mwaka 2008 hadi mwaka huu serikali ilipothibitisha kuwa kweli yana sumu," alisema Makamba.

"Baada ya vipimo kupelekwa kwa mkemia mkuu wa serikali na kubainika yana sumu, leo (juzi) tumefanya ziara na tumethibitisha kuwapo kwa maji haya yenye sumu."

Pamoja na kutozwa faini hiyo, mawaziri hao wameupa mgodi huo wiki tatu kuhakikisha unachimba bwawa jipya la kuhifadhi maji hayo yenye sumu, vinginevyo leseni yake ya uchimbaji itasimamishwa na serikali kuendelea na uchimbaji wa dhahabu.

Makamba alisema serikali imechukua hatua hiyo ya kuutoza faini mgodi huo, baada ya kukiuka sheria na kuwapo uchafuzi wa mazingira na maji yanayotiririka kubainika yana sumu, hivyo kusababaisha wananchi kupata madhara ikiwamo kuugua na kupoteza maisha kutokana na kutumia maji hayo kwa kuoga na kunywa. Pia alisema maji hayo pia yamesababisha mifugo kufa.

Maji hayo yanatiririka kutoka bwawa la mgodi huo la Nyabirama na kwenda kwenye makazi ya wananchi wanaoishi kuzunguka eneo la mgodi, kupitia vijito na Mto Tigiti unaotiririsha maji yake kuingia katika Ziwa Victoria.

Naye Biteko alisema serikali itafanya tathmini upya ya fidia ya madai ya wananchi na mapunjo yao walioathirika na maji ya sumu na wengine kufariki dunia pamoja na mifugo yao kufa kwa vile ina takwimu zote za waathirika hao.

Biteko alisema serikali iko tayari kuwasaidia waathirika wa maji hayo watakapoupeleka mgodi huo mahakamani kudai fidia, baada ya kushindwa kutekeleza kuwalipa kwa hiari fidia zao.

Vijiji vinavyozunguka mgodi huo ni Nyamwaga, Komarero, Genuru, Nakunguru, Kewanja, Kerende, Nyangoto na Nyabichune na viteno kati ya hivyo vinadaiwa kuingia mkataba na mgodi huo ili kunufaika na mapato ya uzaslishaji wa dhahabu mwaka 1995. Vijiji hivyo ni Nyamwaga, Genkuru, Nyangoto, Kerende na Kewanja na kwamba mgodi huo ulianza uchimbaji wa dhahabu mwaka 2000 na kuanza uzalishaji mwaka 2002.

Katika hatua nyingine. Biteko aliitaka migodi yote nchini kuhakikisha inafuata sheria za uchimbaji madini, huku akisisitiza mgodi wa North Mara kufuata taratibu na sheria za uchimbaji pamoja na migodi mingine nchini.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Samwel Gwamaka, alisema baraza hilo litaendelea kusimamia vyema uhifadhi wa mazingira katika migodi yote ya madini nchini ikiwemo kutoa adhabu kwa migodi inayokiuka sheria za uhifadhi wa mazingira.

# Uchaguzi Mkuu 2020 kazi imeanza

**Romana Mallya na Joseph Mwendapole**

JOTO la Uchaguzi Mkuu wa 2020 limeanza kufukuta baada ya vigogo wawili, mfanyabiashara maarufu nchini Rostam Aziz na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, kuanza kurushiana maneno kuhusu uchaguzi huo.

Rostam kwenye ujumbe wa video fupi uliosambaa jana kwenye mitandao ya kijamii, alisikika akimtaka Membe aache harakati zake za kutaka kuwania urais kwenye uchaguzi huo.

Akizungumza kwenye ujumbe huo, Rostam alisema, "Tunajua kwamba hukuwa na uhusiano mzuri naye, lakini hayo tuyaweke kando tumsaidie asiwe na mtu ambaye atachukua fomu kushindana naye," alisema Rostam na kuongeza:

"Nikamwambia Membe huu ni utaratibu ndo mila yetu na desturi ya kuwa mgombea wetu muhula wa pili anakuwa yule yule, hili jambo halina shaka, usisumbuke sana kwa sababu utakuwa mtu wa ajabu sana, mtu ambaye hufikiri vizuri ukiamua kujiingiza na kutaka kuleta vurugu," alisema Rostam.

Rostam alimweleza Membe kuwa uimara wa chama hicho unatokana na mila, desturi na utamaduni wa nani ni wa muhimu wakati wa kuingia kupambana na vyama vingine vya siasa.

"Sasa tukianza na vurugu hizi za watu kujitokeza ni kutaka kufanya fujo tu, hazitusaidii sana katika mapambano yetu dhidi ya vyama vingine," alisema Rostam.

"Membe namfahamu ni mtu ambaye pamoja na yote yale inawezekana anashawishiwa na huyu na yule, lakini hatimaye mheshimiwa Membe ni mtu ambaye ubongo wake ni mzuri, ajue kwamba hili jambo haliendi hivyo."

"Na ninaamini atafika mahali ataunga mkono tiketi yetu ambayo tumekuwa nayo katika miaka mitano ili tupate miaka mitano mingine. Mimi nafananisha masuala haya kama vile mchezo wa mpira, mwaka 2020 zinakuwa dakika 45 zimekwisha tunaingia dakika 45 nyingine ili kuhitimisha hiyo mechi ya mpira," alisema.

Kama kuna kapteni mzuri anayeiendesha timu vizuri hakuna sababu ya kuanza kutoa mtu upande wa mashabiki wanaoangalia mpira kuja kufanya fujo na kutaka kujifanya kapteni.

Alisema mechi ya mpira wa dakika 45 zitafikia mwisho mwaka 2020 na ni lazima wamalize dakika 45 nyingine ili mechi iwe imekamilika kwa kupata kapteni ambaye ataweendesha vizuri.

Kwa upande wake, Membe alipozungumza na waandishi wa habari jana kujibu yaliyosemwa na mfanyabiashara huyo, alisema anapata kigugumizi kumjibu Rostam.

Membe alisema atapanga kukutana na Rostam ambaye ni mchumi ili amshauri kuwa anafanya vizuri katika jamii ya Watanzania anapozungumzia masuala ya uchumi zaidi kuliko siasa.

"Rostam anatakiwa kuzungumzia mambo ya nchi na siyo mambo binafsi ambayo yanatakiwa kuzungumzwa na watu wa chini, kwa nafasi yake anatakiwa kuzungumza masuala ya nchi

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (katikati), akiimba wimbo wa taifa kabla ya kufungua semina ya wanahisa wa Benki ya CRDB, iliyofanyika katika ukumbi wa kimataifa wa AICC, jijini Arusha jana. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela na (kulia kwake) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi CRDB, Ally Laay na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Charles Kichere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge aliyemgomea Ndugai afunguka mazito

**Na Waandishi Wetu**

MBUNGE wa Shinyanga Mjini (CCM), Stephen Masele, amefunguka kuhusu sakata lake na Spika wa Bunge la Afrika, Roger Dang, huku akiwashukuru Watanzania na waafrika wanaomuunga mkono kwenye kadhia hiyo.

Masele ni Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika (PAP), ambaye ameingia kwenye mgogoro na Rais wa Bunge hilo raia wa Cameroon kuhusu rushwa ya ngono.

Masele kwenye ukurasa wake wa Twitter jana aliandika kuwa yeye ataendelea kusimamia haki, ukweli na uadilifu bila woga hadi kieleweke.

"Nawashukuru wote kwa kuniunga mkono nitasimamia haki, mimi ni baba wa mtoto mmoja wa kike siwezi kuvumilia hali hii nawaomba wenzangu wote tupige kelele kuhusu unyanyasaji wa kingono kuanzia shuleni, sehemu za kazi na kwenye jamii tunazoishi na duniani kote," alisema Masele.

Masele alipongeza ushujaa wa wote ambao walijitolea kutoa maelezo kuhusu unyanyasaji uliokuwa unafanywa na Rais huyo wa Bunge la Afrika na kuwataka wengine kuiga mfano huo.

"Nawashauri watu wote wema kupambana dhidi ya unyanyasaji kama huu wa kingono sehemu za kazi, shuleni na jamii nzima Afrika na kwinginеko duniani," alisema Masele.

Alisema hawezi kuvumilia kuona mambo hayo ya kijinga yakiendekezwa kwa kuwa amekulia kwenye malezi ya kuheshimu haki za wengine na maadili.

Kupitia ujumbe wa video fupi iliyosambaa mtandaoni wakati Masele akihojiwa kuhusu tuhuma zinazomkabili Rais wa PAP, alisema amefurahi baada ya kamati ya uchunguzi iliyoundwa na Bunge hilo kuchunguza tuhuma hizo zinazomkabili Rais kukamilisha kazi yake.

"Mimi kama mkuu wa utawala na wafanyakazi wote nina wajibu wa kuhakikisha kwamba hali za wafanyakazi hususan wanawake ambao wanamtuhumu Rais kuwanyanyasa kijinsia, kingono, utafiti unaonyesha kwamba Rais anakesi ya kujibu hivyo tutaikabidhi Umoja wa Afrika kwa ajili ya uchunguzi wa kina," alisema.

Aliongeza kuwa, "Rais anatakiwa apishe ili uchunguzi uweze kufanyika. Ni

INAENDELEA UK. 8



Pikipiki na magari yakikwepa shimo lililopo katikati ya makutano ya Barabara ya Sokoine na Azikiwe, jijini Dar es Salaam jana, kwa muda mrefu sasa na kusababisha usumbufu kwa vyombo vya moto, hali iliyopelekea wasamaria wema kuweka tairi. **PICHA: JOHN BADI**

# Simulizi mume alivyookolewa na samaki kuzama baharini

**Na Boniface Gideon,** TANGA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, mkazi wa Unguja, Hamis Zuberi, amesimulia jinsi alivyookolewa na samaki aina ya papa baada ya jahazi alilokuwa akisafiria kutoka Kipumbwi wilayani Pangani kwenda Unguja kupinduka katikati ya bahari.

Akizungumza na Nipashe katika Hospitali ya Wilaya ya Pangani, Zuberi alisimulia kuwa chombo chao kilipigwa na dhoruba kali ya mawimbi kuanzia majira ya saa sita usiku wa kuamkia Jumapili iliyopita, akiwa yeye, mke wake pamoja na watoto wawili aliokuwa akisafiri nao. "Nilijitahidi kutaka kuokoa familia yangu kwa kutumia gunia la mkaa kwa kuwakalisha juu ya gunia hilo, lakini jitihada zangu ziligonga mwamba baada ya gunia kuchanika na kushuhudia familia yangu ikipoteza maisha," alisema Zuberi.

Alisema wakati akiwa ameketa tamaa, ghafla alitokea samaki aina ya papa na kusogea kifuani mwake na ndipo alipopanda mgongoni mwake na kumsogeza umbali wa mita mia moja karibu na nchi kavu ambako alipiga kelele ya kuomba msaada kwa wavuvi waliopo karibu.

Alisema baada ya kuokolewa na wavuvi walimchukua na kumfikisha katika Hospitali ya Wilaya ya Pangani akiwa hajitambui kutokana na kunywa maji mengi. Aliendelea kusimulia kuwa baada ya kupata fahamu akiwa hospitalini hapo aliwasiliana na ndugu jamaa na marafiki kuhusu hatima ya familia yake ndipo alipoambiwa kuwa mke na mtoto wake mmoja walikutwa wakielea wakiwa wameshakufa na mwingine haijulikani aliko.

"Naumia sana moyoni nimepoteza familia yangu yote," alisema. Kwa upande wake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema watu watano walipoteza maisha na wengine 11 walijeruhiwa katika tukio hilo la jahazi kuzama ambalo lilikuwa limebeba watu 20.

Kamanda Bukombe alisema wengine hajulikani walipo. "Nawaomba wananchi msikubali kupanda vyombo vya baharini ambavyo havijasajiliwa kubeba abiria kwani havina vifaa vya uokoaji," alitahadharisha Bukombe.

# Mambo tisa yatajwa kukipaisha kilimo

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema itafanya mambo tisa katika mwaka ujao wa fedha kwa lengo la kusukuma mbele kasi ya maendeleo ya sekta ya kilimo ili kukibadilisha kilimo kutoka kuwa cha kujikimu na kuwa cha biashara.

Imeelezwa kuwa mambo hayo tisa ambayo ndiyo vipaumbele vya Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha, yamewekwa kwa kuzingatia malengo ya kitaifa katika kufikia kipato cha kati kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana hotuba ya makadirio ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema kilimo ni sekta kubwa na muhimu kwa maendeleo kutokana na mchango wake katika uchumi.

Alibinisha kuwa mwaka 2017, sekta hiyo ilitoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 65.5 na kuchangia asilimia 28.7 ya Pato la Taifa.

Katika hotuba yake hiyo ya kwanza tangu ateuliwe kuwa waziri, Hasunga alisema kipaumbele cha kwanza mwaka ujao wa fedha ni kuongeza tija katika kilimo na upatikanaji wa mbegu bora za kilimo.

Alisema wizara yake itaendelea kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora kwa kutumia rasirimali za serikali, kuishirikisha sekta binafsi na kuongeza udhibiti wa ubora wa mbegu.

"Wakala wa Mbegu kwa kushirikana na sekta binafsi katika mwaka ujao wa fedha, umejipanga kuzalisha tani 3,673.6 za mbegu kutika mashamba yake.

"Wakala kwa kushirikiana na wakulima wa mkataba pamoja na taasisi za serikali kama vile magereza na vituo vya utafiti unategemea kuzalisha mbegu tani 1,246.6," alisema.

Waziri huyo alisema kipaumbele cha pili ni upatikanaji na udhibiti wa ubora wa mbegu, akieleza kuwa wizara itasimamia uagizaji na usambazaji wa tani 625,000 za mbolea zinazokadiriwa kutumika nchini.

Alisema Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) pia itaongeza mauzo ya mbolea kutoka tani 10,000 hadi kufikia tani 100,000.

"Ghala moja lenye kuhifadhi tani 20,000 za mbolea linakarabatiwa mkoani Tabora pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchanganya mbolea kwa uwiano katika Mkoa wa Dar es Salaam," alisema.

Waziri huyo alisema kipaumbele cha tatu cha wizara yake katika mwaka ujao wa fedha ni kuhakikisha upatikanaji wa viuatilifu na udhibiti wa visumbufu.

Hasunga alibanisha kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019, wizara imenunua lita 296,000 na kilo 3,000 za viuatilifu vyenye thamani ya Sh. bilioni tisa ili kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao.

Alisema hadi kufikia Machi mwaka huu, ndege waharibifu

INAENDELEA UK. 8

# JPM atengua uteuzi wa wakurugenzi wawili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ametengua uteuzi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi Mkoani Songwe, Adelius Makwega na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui Mkoani Tabora, Hadija Makuwani.

Ametengua uteuzi wa wakurugenzi hao kuanzia Mei 16, mwaka huu.

Alitangaza uamuzi huo katika kikao cha kazi na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya kilichofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Wakurugenzi wa Halmashauri hizo watateuliwa baadaye.

Wengine waliowahi kutumbuliwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini, Mwantumu Dau, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Erasto Mfugale na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Abdallah Hussein Mussa.

Wakati akifungua mkutano wa 33 wa Jumuiya ya Tawala Mitaa (ALAT), Oktoba 3, mwaka juzi, Rais Magufuli aliwaonya wakurugenzi wanne wa halmashauri nchini wanaojihusisha na ulevi na aliwataka waache mara moja.

"Nimepata taarifa ya Wakurugenzi kama wawili watatu hivi ni walevi sana, nawaambia hao wataondoka kama upo hapa Mkurugenzi halafu ni mlevi ukajirekebishe haraka sana, kabla sijaja huko ili angalau uonekane umebadilika," alionya Rais Magufuli.

Februari 18, 2016 aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), George Simbachawene, aliwasimamisha kazi wakurugenzi wanne wa halmashauri mbalimbali nchini.

Alichukua hatua hiyo baada ya wakurugenzi hao kubainika kutoa rushwa kwa wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), wapewe hati safi kuficha udhaifu katika hesabu zao.

Majina ya wakurugenzi na halmashauri zao kwenye mabano ni Ally Kisenge (Nanyumbu), Abdallah Mfaume (Mbogwe) na mwingine wa Kilolo ambaye hakumtaja jina lake.

Simbachawene pia alimvua madaraka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduma, Halima Mpita, aliyekuwa na tuhuma za kutumia vibaya madaraka yake. Waziri aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuwa Kitundu alikuwa anatuhumiwa kumwagiza Mwekahazina, Majaliwa Byekwaso, kutoa Sh. milioni tatu kwa wakaguzi wa halmashauri hiyo ipewe hati safi.

# Watercom yazalisha ajira zaidi ya 300,000 nchini

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya uzalishaji wa vinywaji ya Watercom Tanzania Limited, imesema inatarajia kuzalisha ajira zaidi nchini Tanzania ili kuendana na kasi ya kukuza uchumi wa viwanda iliyoasisiwa na Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kinywaji kipya cha energy drink kilichoko katika chupa mbili tofauti za Turbo energy drink na Jembe enery drink, Meneja Masoko wa Kampuni hiyo, Shiraz Batchu, alisema mpaka sasa kampuni hiyo imeajiri zaidi ya Watanzania 370,000 nchini katika nafasi tofauti wakiwamo wajasiriamali wadogo.

"Kampuni yetu inayozalisha maji ya afya, energy drink na maziwa ya Dar fresh inajivunia kuzalisha ajira zaidi ya 370,000 ikiwamo ajira za moja kwa moja zaidi ya 2,000 mawakala zaidi ya 3,000 na wajasiriamali wadogo wadogo zaidi ya 350,000 katika kuunga mkono uchumi wa viwanda nchini," alisema Batchu.

Meneja huyo aliwataka Watanzania hasa vijana kuchangamkia fursa kutokana na ubora, urahisi wa upatikanaji na urahisi wa gharama wa bidhaa zake katika kampuni hiyo inayotarajia kuwa na wajasiriamali mara tatu zaidi katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

Meneja huyo alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali kukuza uchumi wa viwanda, mwekezaji wa Kampuni ya Watercom Tanzania aliamua kuanzisha kiwanda kipya cha vinywaji baridi nchini.

Kampuni hiyo pia huwasaidia wajasiriamali kwa kuwapa vitendea kazi kama majokofu na vipoozeo ili kuwapa uwezo zaidi wa kibiashara na kuwaasa vijana nchini kufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na umaskini.



Wananchi wakiangalia basi la daladala, lililochomoka tairi la nyuma, wakati likiwa kwenye mwendo katika Barabara ya Mwananyamala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




## BANDARI YA BAGOMOYO

# Serikali inaendelea na majadiliano ya ujenzi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema inaendelea na majadiliano ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo iliyopo Mkoa wa Pwani ili kuangalia kama kiuchumi itakuwa na tija kwa Tanzania na endapo hawatafikia uamuzi kwenye mambo ya msingi, itaachana nayo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo).

Dk. Abbasi alisema kwa kuwa Tanzania ina ukanda mkubwa wa fukwe ya bahari, serikali ina uwezo wa kujenga bandari nyingi.

"Kuhusu Bandari ya Bagamoyo bado majadiliano yenye tija kwa taifa yanaendelea kufanywa baina ya Serikali ya Tanzania na wawekezaji wa mradi huu. Serikali haijasema mradi wa Bandari hiyo ni hatari, tunaendelea na majadiliano ya utekelezaji wa mradi," alisema.

Dk. Abbasi alikanusha kuwa mradi wa Bandari ya Bagamoyo umeachwa na kueleza kuwa, kuna mambo ya msingi yanajadiliwa na endapo serikali isipofikia mwafaka na wawekezaji itaachana nayo.

Pia alisema serikali haitaacha kuwekeza kwenye maeneo tofauti kwa sababu husaidia maendeleo ya watu na kutolea mfano uwekezaji kwenye sekta ya afya, elimu na miundombinu.

Kuhusu uhuru wa habari na kufungia magazeti yasiyofuata sheria za uchapishaji, Dk. Abbas alisema kuwa ofisi yake haikurupuki kuyafungia magazeti.

"Kati ya magazeti 266 yaliyosajiliwa Tanzania ni magazeti matatu tu yalifungiwa na ninawaomba wamiliki wa magazeti wafuate sheria," alisema. Akitolea ufafanuzi malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu kufunga biashara kwa kisingizio cha kodi na tozo mbalimbali, Dk. Abbasi aliwaeleza kuwa kwa sasa serikali inapita katika kipindi cha mabadiliko na hakuna siku haitadai kodi.

Alisema kodi nyingi zimepunguzwa hususan kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

"Kuna dhana ilijengeka kuwa unaweza kufanya biashara bila kulipa kodi hiyo sasa haipo, lazima tuangalie changamoto ambazo zinakumba sekta mbalimbali mfano sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kulikuwa na kodi zaidi ya 150, serikali imefuta zaidi ya kodi 80 hadi 100," alisema.

# Magari yanayosambaza majisafi kusajiliwa rasmi

**Na Beatrice Moses**

WAMILIKI wa magari ya kusambaza majisafi na majitaka wametakiwa kujisajili rasmi ikiwa ni hatua ya kuwezesha kutoa kwa huduma iliyo bora na salama kwa wateja.

Mamlaka ya Majisafi na na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), imetangaza kuwa itaendesha msako wa kusaka magari ambayo yanatoa huduma hiyo bila kuwa na vibali vya uendeshaji wa huduma hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano cha Dawasa kwa umma jana imebainisha kuwa usajili wa maji hao unatolewa kuanzia Mei 15 hadi 29, mwaka huu.

"Lengo ni kuhakikisha kuwa wateja wanapata maji kupitia magari haya, wanapata huduma bora kutoka vyanzo rasmi vya maji vinavyotambulika na Dawasa," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Miongoni mwa vitu ambavyo magari hayo

INAENDELEA UK. 8

TANGAZO


IPPmedia



IPP Media tunatoa shukurani za dhati kwa Vyombo vyote vya Habari vilivyoshirikiana nasi katika kuchapisha na kurusha mubashara **MSIBA MZITO wa MPENDWA WETU MWENYEKITI MTENDAJI WA IPP - DKT. REGINALD MENGI.**

Aidha tunawashukuru kwa mchango wenu wa hali na mali mliotoa katika kipindi chote cha **MSIBA.**

***Tunasema asante sana kwa:-***

**TV WASHIRIKA:**
1. CLOUDS TV
2. AZAM TV
3. TBC
4. STAR TV
5. CHANNEL 10
6. TV ONE
7. TV E
8. TOP TV UKONGA
9. RISE AND SHINE TV
10. WASAFI TV
11. DIRA TV
12. UPENDO TV

**RADIO WASHIRIKA:**
1. CLOUDS FM
2. MAGIC FM
3. E FM
4. TIMES RADIO
5. RADIO FREE AFRICA
6. RADIO 5
7. PASSION FM
8. PAMBAZUKO FM IFAKARA
9. TOP RADIO MOROGORO
10. HIGHLANDS FM
11. PLANET FM
12. KILI FM MOSHI
13. SUNRISE RADIO ARUSHA
14. UHAI FM
15. UPENDO RADIO
16. WASAFI RADIO

**MITANDAO:**
1. CLOUDS DIGITAL
2. GLOBAL ONLINE TV
3. MILARD AYO
4. MICHUZI BLOG
5. POA TV
6. AZAM DIGITAL
7. WASAFI DIGITAL

**MAGAZETI:**
1. MWANANCHI/THE CITIZEN
2. DAILY NEWS/HABARI LEO
3. MTANZANIA
4. TANZANIA DAIMA
5. GLOBAL PUBLISHERS
6. UHURU/MZALENDO
7. JAMHURI
8. MAJIRA
9. TAZAMA

***Na kwa wengine wote walioshiriki nasi kwa njia moja au nyingine tunasema AHSANTE SANA NA MUNGU AWABARIKI.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utulivu wahitajika zaidi kipindi cha usajili nchini

**WAKATI** msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa mwaka 2018/19 ukielekea ukingoni, hizo ni dalili za wazi kuwa maandalizi ya msimu mpya yanatakiwa kuanza mara moja.

Msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara unatarajiwa kumalizika ifikapo Mei 28 mwaka huu kwa timu zote 20 zinazoshiriki ligi hiyo, kushuka dimbani kuwania pointi muhimu.

Hata hivyo wakati ligi hiyo ya juu kwa upande wa Tanzania Bara ikiwa inakaribia kumalizika, mbio za kuwania ubingwa zimebaki kwa timu mbili tu ambazo ni vigogo, Simba na Yanga.

Simba ambayo imecheza mechi 34 ina pointi 85 na imebakiza michezo miwili wakati Yanga iliyoko katika nafasi ya pili imeshuka dimbani mara 36 ikiwa na pointi 83, wamebakiza mechi mbili huku Azam ambayo pia imebakiza mechi mbili ina pointi 69.

Tayari timu ya African Lyon ya jijini Dar es Salaam yenye pointi 22 inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo hata kama itafanikiwa kushinda mechi zake mbili za mwisho zilizobakia.

Jambo kubwa la kwanza ambalo ni muhimu katika maandalizi ya msimu mpya ni mchakato wa usajili.

Nipashe linapenda kuwakumbusha wachezaji kuwa makini katika kipindi hiki kwa sababu mara nyingi klabu huangalia zaidi maslahi yake badala ya mchezaji ambaye humtegemea kuja kuwatumikia.

Pia viongozi wa klabu nao wanatakiwa kutokurupuka kuingia mikataba bila ya kuwasiliana na timu ambayo anatoka mchezaji huyo mpya wanayemhitaji.

Kwa kufuata utaratibu huu, maneno au kauli za kupishana hazitaweza kusikika kama ambavyo imekuwa ni kawaida kutokosekana kwa mchezaji kusajiliwa, hali ya kuwa bado hajamaliza mkataba na timu yake ya zamani.

Imefika wakati gazti hili linawakumbusha wachezaji na viongozi kukamilisha mchakato huu kisasa na hii itamaliza migongano isiyo ya lazima au itaifanya kamati husika kutofungia mchezaji, kwa sababu inaamini kucheza mpira ndio kibarua pekee cha wachezaji wetu ambao nao wana familia na wazazi wanaowategemea.

Umakini ndio humaliza sintofahamu kwa klabu zetu pamoja na wachezaji kwa kila upande kuheshimu makubaliano yaliyopo katika mkataba.

Tayari imeshaanza sintofahamu ya usajili wa mshambuliaji wa Yanga, Heritier Makambo, ambayo inaelezwa kuwa tayari ameshasaini mkataba wa kujiunga na Horoya FC ya Guinea, wakati mwenyekiti wake, Dk. Mshindo Msolla akisema kwamba bado ni mchezaji wao halali.

Hapa ndipo umakini unapochukua nafasi, inawezekanaje mchezaji ambaye klabu inasema ina mkataba naye utakaomalizika Juni mwakani kusajiliwa na timu nyingine, huku ikielezwa kwamba si mali yao bali ni mchezaji wa FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Huu ni mwanzo, Nipashe inawakumbusha wachezaji na viongozi kutokurupuka katika mchakato huu ambao kama klabu au mchezaji atafanya kosa, basi atakuwa amejiweka mwenyewe katika kifungo kwa msimu mmoja au miwili kulingana na mkataba ambao atakuwa amesaini.

Vile vile ni muda kwa wasimamizi wa soka nchini (TFF) kuendelea kuhakikisha wachezaji wa kigeni watakaosajiliwa wanakuwa na viwango vya juu na si kuruhusu "wajanja" kutumia Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa sehemu ya majaribio au kujiimarisha kwa sababu hili halitasaidia kuwaendeleza wachezaji wazawa na badala yake itakuwa inajaza nafasi zao bure.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Fadhila za punda mateke!



Na Barnabas Maro

**UKIMTUNZA** punda vizuri atasahau na (ashaakum) kukujambia au hata kukupiga mateke unapomkaribia!

Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu anayetendewa wema na badala ya kuurudisha wema aliotendewa akawa anarudisha ubaya. Huweza kutumiwa kwa mtu asiyekuwa na shukrani.

Kuna mtu anayeitwa Jella Mtagwa. Huyu alikuwa mchezaji kabumbu mahiri wa timu ya Yanga jijini Dar es Salaam aliyesajiliwa kutoka 'mji kasoro bahari' (Morogoro). Kwa uhodari wake wa kusakata kabumbu, akateuliwa kuwa nahodha wa Yanga na pia Timu ya Taifa (Taifa Stars).

"Mcheza kwao hutuzwa" chambilecho wahenga. Maana yake mtu anayecheza kwao hupewa zawadi au hutunzwa vizuri. Methali hii hutumiwa kutufunza kwamba mtu anayefanya jambo vizuri au inavyopasa, hutuzwa au hupewa zawadi.

Ndivyo alivyofanyiwa Jella Mtagwa kwani Shirika la Posta na Simu (au Serikali?) iliamua kumtuza kwa kuweka picha yake kwenye stempu zilizotumika kwenye barua. Hapana shaka barua zilizotumwa ndani na nje ya nchi zilifanya ajulikane na wengi na kufahamika kwa umaarufu wake.

Ingekuwa ni wakati wa sasa ambapo timu za Ulaya zinatafuta wachezaji kutoka Afrika, hapa shaka leo hii angekuwa mmoja wa wachezaji walionufaika kucheza Ulaya na kuishi maisha mazuri ya uhakika. Si ajabu tungekuwa tunamzungumzia tofauti na alivyo sasa lakini hakubahatika.

Matokeo yake, bidii na fadhila zote alizozitendea nchi yake kupitia Yanga, Shirikisho la Soka Nchini na Serikali, vyote havimkumbuki!

Hii yanikumbusha walivyosema wahenga kuwa "Kuku wa mkata hatagi, akitaga haangui, akiangua hutwaliwa na mwewe." Maana yake kuku wa maskini hatagi na hata akitaga hafanikiwi kuwatunza wale vifaranga.

Nilipata mshtuko na simanzi nilipoona picha ya Jella Mtagwa akiwa kazungukwa na mkewe na baadhi ya watu waliokwenda kumjulia hali nyumbani kwake. Ilikuwa vigumu kumtambua mara moja kwa jinsi alivyodhoofika kutokana na maradhi yanayomsumbua.

Huyu ni mtu aliyeitumikia Yanga kwa mafanikio makubwa enzi zake lakini katika watu waliokuwa naye siku ilipotangazwa na runinga, sikumwona kiongozi yeyote wa Yanga. Ingawa hawakuwepo enzi zake walipaswa kumtembelea mara kwa mara na kumpa msaada wakikumbuka juhudi zake alipokuwa mchezaji wa klabu hiyo maarufu nchini.

TFF nalo lipo kimya kuhusu mchezaji huyo wa zamani kama lilivyo Shirika la Posta na Serikali pia! Ni kama kusema "Iliyopita si ndwele (kitumbe cha mongo), tugange yajayo." 'Kitumbe cha mongo' ni usemi wa zamani wenye maana ya kitu cha kutupwa mgongoni.

Jambo lingine la kufanyiwa kazi ni wachezaji kuwa na chama imara kitakachowatetea na kuwasaidia wanapodhulumiwa haki zao au kutopewa mishahara na stahiki zao kwa muda mwafaka. Mara nyingi wachezaji hulipwa fedha zao za usajili, na mishahara kwa mafungu tena baada ya kudai kwa mbinde na kutishia kuachana na klabu.

Kadhia hii husababisha baadhi ya wachezaji kuzisusa timu zao kama ilivyokuwa kwa mshambuliaji Obrey Chirwa aliyekuwa Yanga na sasa yupo Azam. Pia Beno Kakolanya aliyekuwa kipa namba moja wa Yanga ambaye mkataba wake umemalizika akisusa kuwa kwenye kikosi cha Yanga kwa kudai malimbikizo ya mishahara yake.


Ucheleweshaji na ubabaishaji wa stahiki za wachezaji huwaogofya hata wanaotaka kujisajili na Yanga kila wanaposikia ubabaishaji wanaofanyiwa wenzao wa klabu hiyo. Siku hizi mchezo wa mpira ni kazi kama zilivyo zingine. Mfanyakazi hufanya kazi kwa uangalifu na bidii akitegemea kulipwa mshahara wake mwisho wa mwezi.

Fedha hizo humsaidia kulipa kodi ya nyumba, ada za shule kwa watoto wake, chakula na mahitaji mengine muhimu. Sasa kama halipwi mshahara wake kila mwezi ataishi vipi? Awe omba omba? Hili ndilo linalowakatisha tamaa wachezaji wengi kusajiliwa na klabu isiyolipa mishahara kwa wakati.

Jambo hili na mengine yaangaliwe kwa makini na viongozi wapya wa Yanga waliochaguliwa hivi karibuni. Wanapaswa kufanya mambo kwa vitendo badala ya maneno matupu.

Nimalizie makala yangu kwa maneno waliyotuachia wahenga kuwa: "Ahadi ni deni (na deni ijuzie)." Maana yake ahadi ni kama deni, mtu akitoa ahadi lazima aitimize. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutimiza ahadi tutoazo.

**marobarnabas@yahoo.com 0784 334 096**



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka

# Bil. 30/-zajenga maboma ya shule

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema katika mwaka wa fedha 2018/19, serikali imetoa Sh. bilioni 29.9 kwa ajili ya ukamilishaji maboma 2,392 ya shule za sekondari.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Mwita Waitara, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Solwa (CCM), Ahmed Salum. Mbunge huyo alisema katika jimbo lake tayari kuna maboma 158 yakiwamo ya shule za msingi, sekondari na afya na tayari walishaomba fedha ili kukamilisha maboma hayo.

"Je, ni kiasi gani cha fedha jimbo langu limepata ili kukamilisha maboma hayo?" alihoji.

Pia alitaka kujua mpango mkakati wa serikali kukamilisha maboma hayo ambayo yanahitaji Sh. bilioni 4.7. Akijibu maswali hayo, Waitara alisema katika kiasi hicho cha fedha, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imepatiwa Sh. milioni 87.5 kwa ajili ya kukamilisha maboma saba ya shule za sekondari. "Serikali imepeleka Sh. bilioni 29.9 nchi nzima na majimbo yote yamepata. Suala la kumalizia maboma ni jambo mtambuka na tunahusisha wadau mbalimbali ili kukamilisha," alisema.

Aidha, Waitara alisema serikali inaendelea na ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati 352 kwa gharama ya Sh. bilioni 184.6 na kwamba kipaumbele ni ukamilishaji wa maboma yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi. "Ukarabati wa vituo hivi unahusisha ukamilishaji wa maboma 199 ya vituo vya afya na zahanati, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Serikali imefanya ukarabati wa vituo vya afya vya Samuye na Tinde kwa gharama ya Sh. milioni 900,"alisema.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 kupitia mapato yake ya ndani, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imetenga Sh. milioni 140 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati.

# Mbeya sasa kutoa tiba saratani

SERIKALI imesema iko katika mpango wa kufungua huduma za tiba ya saratani kwenye Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya ili kuipunguzia mzigo Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.

Sambamba na mpango huo, imesema iko mbioni kuanzisha programu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama ilivyo kwa Ukimwi, kifua kikuu na maralia.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk.Faustine Ndugulile, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Dau Haji.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mpango gani katika kushughulikia magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu na kansa ambayo yanawapa shida kubwa ya kiafya.

Akijibu swali hilo, Dk.Ndugulile alisema lengo la kuanzisha programu hiyo ni kufikisha huduma hizo hadi ngazi ya zahanati na kuzipa mwonekano wa kipekee huduma za magonjwa hayo.

Alifafanua kuwa magonjwa hayo yamekuwa wakiongezeka duniani kote ikiwa ni pamoja na nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwamo, na hali hiyo ilianza miaka ya 1990.

Aidha, alisema serikali kupitia Sera ya Afya ya mwaka 2007 ilitoa tamko la kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Naibu Waziri alisema mwaka 2009 serikali kupitia Wizara ya Afya, ilianzisha kitengo cha kushughulikia magonjwa hayo na kutengeneza mpango mkakati wa mwaka 2009 hadi 2015 na sasa wanatekeleza mpango wa mwaka 2016 hadi 2020.

"Serikali imeboresha huduma za magonjwa ya moyo, ikiwamo shinikizo la damu kwa kufungua Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Ocean Road, Bugando, KCMC na Benjamini Mkapa," alisema.

Alitoa rai kwa wananchi kuhakikisha wanajikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa kufanya mazoezi angalau mara tatu kwa wiki, kula mlo unaofaa, kutotumia tumbaku na bidhaa zake na pia kupunguza matumizi ya pombe.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kufanya matibabu hayo kuwa bure kwa watu wasio na bima ya afya.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema magonjwa hayo yana gharama kubwa na ni ya kudumu.

"Kwa mfano tatizo la figo ili mgonjwa asafishe damu kwa wiki anahitaji kati ya Sh. 750,000 na milioni moja na kupandikiza figo hapa nchini takribani Sh. milioni 20, kisukari anahitaji Sh.50,000 hadi Sh.100,000 ,"alisema.

Alisema serikali ili kutoa nafuu kwa wananchi, inaelekea kwenye bima ya afya kwa wananchi wote.

# Mbunge alia daraja lililosombwa na maji

MBUNGE wa Mpwapwa (CCM), George Lubeleje, ameitaka serikali kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Godegode ambalo lilisombwa na maji wakati wa mvua na kukata mawasiliano kati ya jimbo hilo na Kibakwe.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge huyo alisema daraja lililosombwa na maji lilijengwa kwa Sh. milioni 500 na kwamba daraja lingine linalotarajiwa kujengwa litagharimu Sh. milioni 325 kiasi ambacho hakitoshi.

"Leo mnajenga hilo daraja la Sh. milioni 325 si ndiyo litachukuliwa mapema? Kwa nini msiongeze fedha Mheshimiwa Naibu Waziri?" alihoji.

Pia katika swali la msingi, Lubeleje alisema daraja hilo ni kiungo kikubwa cha majimbo hayo na kutaka kujua serikali ina mpango gani wa kujenga daraja hilo ili kurejesha mawasiliano kwa wananchi wa kata za Godegode, Pwaga, Lumuma, Mbuga na Galigali.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alikiri kuwa daraja hilo lilisombwa kipindi cha masika mwaka jana na serikali ina mpango wa kurejesha mawasiliano hayo kwa kujenga daraja jipya.

"Ujenzi wa daraja hilo utaanza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambapo kiasi cha Sh. milioni 325 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo,"alisema.

Kuhusu fedha kutotosheleza, Kwandikwa alimtoa mashaka Mbunge huyo kwa kudai kuwa kazi hiyo itafanyika vizuri.

"Tumetenga kwa ajili ya usanifu Sh. milioni 325 na baada ya hapo tutaanza kujenga na kuna Sh. milioni 180 zingine zimetengwa, tumejipanga kujenga daraja hili na litakuwa daraja bora," alisema.




**Na Augusta Njoji,** DODOMA

# Mbunge aliyemgomea Ndugai afunguka

INATOKA UK. 2

uchunguzi ambao umekuja na ushahidi ambao umethibitisha kwamba amefanya hivyo na yeye mwenyewe amekiri amefanya, ameomba msamaha, lakini haitoshi lazima uchunguzi zaidi ufanyike ili kukomesha tabia hii," alisema.

"Wewe Rais wa Bunge unatumia mamlaka yako vibaya kumwandikia Spika wa Bunge la Tanzania kwamba nirudi nyumbani, mimi sirudi kwasababu sikuchaguliwa na wewe, hawa waheshimiwa wabunge ndio walinichagua na ndio wenye mamlaka ya kuniondoa," alisema Masele

**ALICHOSEMA NDUGAI**

Juzi, Spika Ndugai, alitangaza bungeni kusitisha uwakilishi wa Mbunge Masele (CCM) katika Bunge la Afrika (PAP) kutokana na tuhuma za utovu wa nidhamu.

Masele ambaye katika serikali ya awamu ya nne alikuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini na baadaye Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa PAP.

Kutokana na uamuzi huo wa Spika Ndugai, Masele ambaye kwa sasa yuko nchini Afrika Kusini kwenye vikao vya PAP, ametakiwa kurejea nchini ili kuhojiwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge huku akidokeza kuwa hata Kamati ya Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) nayo itamhoji.

Ndugai alisema katika uwakilishi wa Masele kwenye Bunge hilo la Afrika, kumejitokeza matatizo makubwa ya kinidhamu.

Kiongozi huyo wa Bunge la Tanzania alidai Masele ni kiongozi ambaye amekuwa akifanya mambo ya ovyo ovyo ndiyo maana ameitwa kwenye Kamati ya Maadili.

"Tumemwita aje atufafanulie, huenda yuko sahihi, lakini kwa mtazamo wetu, tunaona anafanya mambo ya hatari ikiwamo kugonganisha mihimili," Ndugai alisema.

"Amekuwa akipeleka mhimili wa juu kabisa wa serikali maneno mengi ya uongo na kudhalilisha Bunge na ushahidi upo. Ni kiongozi ambaye amejisahau, sijui anatafuta kitu gani. "Hizo vurugu ambazo anazionyesha kwenye Bunge lake huko, sisi hazituhusu sana. Tumemwita aje kwa mambo ya hapa nyumbani ya utovu wa nidhamu.

"Kwa kuwa tumekuwa tukimwita hapa nyumbani tangu Jumatatu hataki kurudi, nimemwandikia barua Rais wa PAP ya kusitisha uwakilishi wa Stephen Masele katika Bunge la PAP hadi hapo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itakapokamilisha uchunguzi na tuhuma dhidi yake."

**MSIGWA AHOJI**

MBUNGE wa Iringa Mjini, Mch. Peter Msigwa (Chadema), amehoji nafasi ya wabunge wanaochaguliwa na Bunge kuliwakilisha katika mabunge mengine duniani, kusimamishwa na Kiti cha Spika bila uamuzi huo kujadiliwa na waliowachagua.

Baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jijini Dodoma jana asubuhi, mbunge huyo alisimama na kuomba mwongozo kwa Mwenyekiti wa Bunge, Andrew Chenge aliyekuwa anaongoza kikao, akihoji uhalali wa Kiti cha Spika kuwasimamishwa wawakilishi waliochaguliwa na chombo hicho cha kutunga sheria.

"Uhalali unatoka wapi na hawa hawakuteuliwa, wamechaguliwa? Na nilitaka kujua anasimamishwa na kiti bila kujadiliwa, inatuchafua kama taifa. Bunge litakuwa na nguvu gani ya kuwalinda hawa tunaowachagua?" Mch. Msigwa alihoji.

Mbunge huyo alisema ameona ahoji kuhusu suala hilo baada ya juzi Spika wa Bunge, Job Ndugai, kutangaza kusimamisha uwakilishi wa Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele (CCM) katika Bunge la Afrika (PAP) akimtuhumu kwa utovu wa nidhamu.

Akimjibu Mch. Msigwa, Mwenyekiti wa Bunge, Chenge, alimtaka mbunge huyo kutowahisha hoja kwa kueleza kuwa tayari Spika Ndugai amelitolea uamuzi suala hilo.

Chenge ambaye aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aliwataka wabunge kusubiri hadi taarifa ya suala hilo itakapowasilishwa bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na watakuwa na nafasi ya kujadili. Alisema kwa sasa milango bado haijafungwa kwao kulijadili suala hilo, lakini ni lazima taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge zifuatwe.

Kiongozi huyo wa Bunge la Tanzania pia alieleza kuwa baada ya kumalizana na kamati ya Bunge, Masele pia atahojiwa na Kamati ya Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na tuhuma za utovu wa nidhamu.

■ **Imeandikwa na Joseph Mwendapole na Romana Mallya, DAR na Sanula Athanas, DODOMA.**

# Mambo tisa yatajwa

INATOKA UK. 3

wa nafaka walidhibitiwa katika skimu za umwagiliaji za Kahe, Lekitatu na Misenyi kwa mazao ya mpunga na mtama.

Aliongeza kuwa lita 119,000 kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi vamizi zimesambazwa Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki na kutoa mafunzo kwa maofisa ugani na wakulima 350.

Hasunga ambaye pia ni Mbunge wa Vwawa, alisema kipaumbele cha nne cha wizara hiyo ni kujikita katika upatikanaji wa zana za kilimo. Alisema takwimu zinaonyesha wastani wa kitaifa wa matumizi ya zana bora za kilimo umeongezeka hadi kufikia asilimia 20 kwa matrekta na asilimia 27 kwa wanyama kazi ikilinganishwa na asilimia 14 ya matrekta na asilimia 24 ya wanyama kazi mwaka 2013.

Alisema kutokana na ongezeko hilo, matumizi ya jembe la mkono yamepungua na kufikia asilimia 53 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 62 kwa mwaka 2013.

"Kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF), wizara imeendelea kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu, mikopo 33 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.50 imetolewa," alisema.

Alisema kipaumbele cha tano ambacho serikali imejielekeza kwenye sekta hiyo ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji.

Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Umwagiliaji, alisema imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo unaofadhiliwa na serikali ya Japan.

Alisema mradi huo umekarabati skimu za umwagiliaji 129 katika halmashauri 68 nchini pamoja na ununuzi wa mitambo ya uenjzi.

Kipaumbele cha sita cha wizara hiyo ni utafiti wa kilimo na uhaulishaji wa teknolojia, ikibainisha kuwa katika mwaka 2018/2019, wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari), imegundua mbegu bora mpya aina nne za mahindi. Alisema mbegu hizo zina uwezo wa kutoa mavuno kwa wastani wa tani 5.8 kwa hekta kwenye mashamba ya wakulima katika ukanda wa chini na kati, zinahimili ukame na zina ukinzani wa magonjwa ya majani ya mahindi, michirizi na ukungu.

"Vilevile, kwa kushirikiana na kampuni binafsi, Tari imezalisha aina sita ya miche ya mbegu bora ya migomba na kugundua aina 62 za mbegu za mazao ya mikunde," alisema.

Hasunga alisema kipaumbele cha saba cha wizara yake ni kujikita katika kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao mbalimbali kwa kuimarisha huduma za utafiti, upatikanaji na utumiaji wa pembejeo na zana za kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mazao, huduma za ugani, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko.

Alisema wizara imeandaa mkakati wa miaka minne (2018/2019 - 2021/2022) wa kuendeleza zao la michikichi.

Hasunga alisema kipaumbele cha nane ni kuimarisha miundombinu ya hifadhi na uongezaji thamani mazao ya kilimo.

Waziri huyo alisema kipaumbele cha tisa cha wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha ni kuimarisha huduma za utafiti na ushirika, akibainisha kuwa watakarabati ofisi na kuvipatia vifaa muhimu vituo vya utafiti vya Ukiliguru, Ilonga na Tumbi.

Alisema miundombinu ya umwagiliaji ya vituo vya utafiti vya Ilonga, Naliendele, Ukiliguru na miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Seliani pia itaboreshwa.

# Magari majisafi

INATOKA UK. 4

yanapaswa kuwa navyo ni pamoja na nakala ya leseni ya dereva, kadi ya gari, bima ya gari na kuthibitishwa na mwanasheria.

Imebainishwa katika taarifa hiyo kuwa baada ya muda wa usajili kuisha gari lolote la majisafi litakalokuwa katika eneo la huduma la Dawasa likitoa huduma bila leseni ya uendeshaji, wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Kuhusu majitaka, Dawasa imebainisha kuwa lengo ni kuhakikisha kuwa magari yanayobeba maji hayo yanayonya na kumwaga kwenye mabwawa ya kutibu majitaka yanayomilikiwa na mamlaka hiyo.

Hatua hiyo imepongezwa na wakazi kadhaa wa Wilaya ya Ubungo jijini hapa, wakieleza kuwa itawahakikisha usalama wa maji wanayonunua kutoka kwenye magari hayo.

" Binafsi naishi katika eneo la Golani bado hatujafungiwa maji hivyo tunategemea maji yanayouzwa katika magari haya, lakini hatuna uhakika na usalama wa maji yenyewe wakati mwingine tunauziwa yana chumvi tena kali hata ikipikwa chai ukinywa unaisikia, pia madumu mengine yameota ukungu wa kijani hatua hii ya Dawasa inaonyesha wameamua kulinda usalama wa afya zetu," alisema Belinda Julias.

# Uchaguzi Mkuu 2020 kazi imeanza

INATOKA UK. 2

siyo masuala binafsi," alisema na kuongeza:

"Kwa nafasi zetu tunatakiwa kuzungumzia masuala ya kitaifa yanayohusu uchumi, kwanini uchumi upo hapa ulipo? Kwanini wafanyabiashara wadogo na wakubwa wanafunga biashara? Au zile alizozieleza za watu wanaopotosha kuhusu mwenendo wa kiuchumi," alisema.

"Rostam wewe ni mwenzetu sisi, tumekatwa mikia, ukikatwa mkia hata ujitahidije mkia wako ni mfupi tu, tunayoyazungumza ni vizuri tuwe na misimamo kwenye dhamira yetu na tunayoyazungumza midomoni, tuwe tunazungumza kitu ambacho binadamu atatuheshimu," alisema.

"Rostam tuzungumzie masuala ya uchumi wa nchi yetu haya yatampa heshima kubwa kuliko kujaribu kujifanya mtoto mzawa badala ya kukubali hali ya halisi kwamba mimi na yeye ni watoto wa kambo," alisema Membe.

**Rostam Aziz ni nani?**

Alikuwa Mbunge wa Igunga (CCM), Tabora hadi mwaka 2011 alipoamua kuachana na shughuli za siasa alizoziita majitaka, ni mfanyabiashara, mchumi na mjasiriamali ambaye jarida la Forbes liliwahi kukadiria kuwa utajiri wake unafikia dola bilioni moja.

Aliwahi kuwa Mweka Hazina wa CCM 2005 hadi 2007 alianza kuongoza Jimbo la Igunga mwaka 1994 na akawa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM kuanzia mwaka 2006 hadi 2011 alipoamua kuachia nyadhifa zake zote.

Rostam alifanikiwa kuingia bungeni mwaka 1994 akiwa na miaka 26 na kuwa mbunge kijana kuliko wote, aliamua kuachama na siasa baada ya CCM kuanzisha utaratibu wa kujivua gamba.

Mwishoni mwa mwaka jana Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally alikuwa kiongozi wa kwanza mkubwa wa CCM kwa kukemea wanaoanza kujipitisha pitisha kwaajili ya uchaguzi mkuu wa mwakani.

**Bernad Membe**

Mwaka 1978, Membe alipata mafunzo ya Sheria za Jinai na Usalama wa nchi, nchini Uingereza. Alipata mafunzo ya siasa, katika Chuo cha Chama cha Mapinduzi (CCM), Kivukoni, Dar es Salaam.

Alitumikia nafasi mbalimbali ikiwamo Kamanda wa Vijana wa Mkoa wa Lindi, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa na Katibu wa Secretariati ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

Mwaka 2000, aliingia bungeni baada ya kuchaguliwa Jimbo la Mtama.

Alikuwa mchangiaji mkubwa wa mijadala inayohusu amani, ulinzi na usalama pamoja na utawala bora.

Aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alimteua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Kufuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri Oktoba, 2006, Bernard Membe alihamishwa wizara na kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Nishati na Madini

Januari 2007, alimteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa baada ya aliyekuwa anashikilia wadhifa huo Dk Asha Rose Migiro kuteuliwa na Katibu Mkuu Baraza la Umoja wa Kimataifa na kuwa Naibu Katibu Mkuu wa baraza hilo.

Alihudumu katika nafasi hiyo tangu 2007 hadi 2015, akiwa ni Mtanzania wa pili kushika wadhifa huo kwa miaka mingi mfululizo, akitanguliwa na Kikwete ambaye alidumu katika Wizara hiyo kwa miaka 10 mfululizo.

Kwa kutambua mchango wake katika kurejesha hali ya amani na utulivu katika Visiwa vya Comoro, mwaka 2008, Bernard Membe alikuwa miongoni mwa Watanzania waliotunukiwa Nishani ya Operesheni Demokrasia Comoro.

# TCAA yatoa tahadhari watumia ndege zisizo na rubani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imewataka watumiaji wa ndege zisizokuwa na rubani, kufuata sheria, kanuni na taratibu, wakati wa kurusha ndege hizo ili kuepusha ajali.

Akizungumza jana na wandishi wa babari Mkoa wa Arusha, wakati wa kutoa mafunzo ya kujengea uwezo wa kuandika habari za usafiri wa anga, Mkaguzi wa Operesheni za safari za ndege nchini, William Zelothe, aliwataka watu wote kufuata sheria, wakati wanaporusha ndege hizo angani ili kuepusha ajali zisizokuwa na ulazima kutokea.

Alisema kuna baadhi ya watumiaji wa ndege hizo, wamekuwa wakirusha ndege hizo umbali wa zaidi ya futi 500 wakati hazitakiwi, hivyo husababisha mwingiliano na ndege za kawaida.

"Ndege zisizokuwa na rubani zinatakiwa kutorushwa umbali mrefu na baadhi ya watumiaji wamekuwa wakizirusha umbali wa zaidi ya futi 500, kitendo ambacho kinaweza kusababisha mwingiliano na ndege za kawaida, wakati zikitua na kusababisha ajali," alisema Zelothe.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Ofisi ya Rais Tamisemi, wameanzisha utaratibu wa kufuatilia, kusimamia na utaratibu wa uingizaji na matumizi ya ndege hizo kwa lengo kulinda usalama wa anga.

Alisema ndege zisizokuwa na rubani, zimekuwa zikitumika katika masuala ya ulinzi, kupiga picha, katika kilimo kwa ajili ya kumwagilia mimea, kufanya tafiti, kukagua mapori na kupeleka dawa maeneo yasiyofikika kwa urahisi.

Aidha, alisema kwa watu watakaohitaji kurusha ndege hizo umbali mrefu wanapaswa kuandika barua kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, wakieleza aina ya kazi wanayotaka kufanya, aina ya ndege, shughuli itakapoanzia na itakapoishia, kukilipia chombo hicho bima pamoja na kutaja jina la mtu atakayerusha ndege hiyo.

Alisema baada ya kukidhi vigezo hivyo, wahusika watasubiri kwa muda wa siku 60, ndipo watapatiwa kibali, lakini kama ni mgeni kutoka nje ya nchi, atalipia fedha ambazo ni Dola 100.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha, Claud Gwandu, aliishukuru mamlaka hiyo, kwa kutoa mafunzo kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Arusha.

Alisema mafunzo hayo, yatawajengea uwezo na uelewa waandishi wa habari, katika sekta ya anga na kuwataka watoe elimu hiyo kwa wananchi ili kutambua masuala ya anga.




Diwani wa Viti Maalum wa Tarafa ya Haydom katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Elizabeth Hhari, akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wachimbaji waagizwa kujenga uzio eneo la migodi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WACHIMBAJI wa Madini ya Tanzanite wa Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wameongezewa mwezi mmoja ili wakamilishe shughuli ya kuweka uzio kwenye migodi yao na kuvunja mabanda ya soko yaliyopo migodini kwa lengo la kuanzisha soko moja.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, akizungumza jana alisema awali walitoa muda wa mwezi mmoja, lakini wameombwa waongezewe mwezi mwingine.

Ntalima alisema kila mgodi uliopo kwenye machimbo ya madini ya Tanzanite unatakiwa kujenga uzio sababu ya usalama hivyo wameongeza muda.

Alisema suala la kuhamisha masoko kwenda kwenye eneo moja limefikia asilimia 30 na watu wanaendelea kuhamishia mahali walipoelekezwa. Alisema kwa upande wa vyoo kwenye machimbo hayo walitarajia kuwa na matundu 16 ikiwamo kitalu D matundu nane na kitalu B (Opec) matundu nane pia yataongezwa yawe 32 na utaratibu unaenda vizuri. "Nadhani muda huo unatosha kila mmoja kutimiza wajibu wake na mabanda yanayopaswa kuvunjwa yamewekwa alama X tunataka hayo yafanyike ili tubaki kusimamia migodi pekee," alisema Ntalima.

Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji madini mkoani Manyara (Marema), Tawi la Mirerani, Shwaibu Mushi aliwataka wamiliki wa migodi kutekeleza maagizo hayo ya serikali kwa kutii bila shuruti. Mushi alisema bado wachimbaji wanapaswa kusajili wafanyakazi wao kwenye ofisi ya Marema ili watenda kazi wafahamike kupitia usajili huo.

Mmoja kati ya wachimbaji wa eneo hilo (MwanaApolo) Johnson Mwakasege, alisema itakuwa vyema endapo migodi ikiwa na uzio kwa kuwa hali ya usalama wa eneo husika itakuwa ya uhakika.

Mwakasege alisema baadhi ya wachimbaji wanaonekana kususia migodi yao kwa kuwa mingine imeachwa wazi kwa kutokuzibwa midomo hivyo kwa agizo hilo wamiliki watafanyia kazi.

## Waandishi watakiwa kuelimisha athari mitandao ya jamii

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WAANDISHI wa habari wametakiwa kufunguka na kueleza ukweli wa athari kubwa inayoendelea kushika kasi ya mitandao ya jamii kwa Watanzania kutokana na kurusha habari bila kuhaririwa kitaaluma.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jimbo Kuu la Arusha la Kanisa Katoliki Padri Faustine Mosha, alisema hayo wakati akifungua semina kwa waandishi wa habari kuhusu majukumu ya mwandishi wa habari katika zama za mitandao ya jamii iliyofanyika mjini hapa jana.

Padri Mosha, alisema hivi sasa kila mtu amekuwa mwandishi wa habari ilimradi anamiliki simu ya kisasa na kurusha picha ama habari yoyote anayoipata bila ya kuzingatia maadili ya uandishi wa habari.

Alisema hivi sasa katika mitandao hiyo kumeshuhudiwa picha ambazo kimsingi hazifai kurushwa katika jamii zikiwamo za mauaji ya kutisha, zenye kuchochea uhasama na za vitendo vya ngono.

"Nyinyi waandishi wa habari wenyewe ndiyo mnajukumu la kupaza sauti na kukemea hali hii kwa ajili ya ustawi wa jamii yetu na endapo mtanyamaza kimya kuna siku hamtakuwa salama kwani mtasutwa na jamii nzima," alisema.

Alisema, endapo jamii inahitaji kupata habari zinazopitia kwenye mitandao ya kijamii ni vyema pakawapo na utaratibu ambao mitandao hiyo itakuwa na wahariri ambao watazingatia sheria na taratibu za upashanaji wa habari.

Padri Mosha alisema mitandao hiyo inaendesha shughuli zake bila kikomo wala kikwazo chochote na tayari imeanza kuonyesha mwelekeo mbaya kwa kuwa kuna baadhi ya watu wameshaumizwa na habari za uzushi.

Kwa upande wake mwezeshaji wa semina hiyo, Florence Mustapha, aliwataka waandishi wa habari kubaki kwenye misingi ya taaluma yao ya kuhabarisha kwa kuzingatia ukweli na kamwe wasikubali kuvutika na shinikizo la mitandao ya jamii.

# Mapya yaibuka mkataba kampuni za mafuta

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAPYA yameibuka siku chache baada ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Moshi kuamuru biashara katika kituo cha mafuta kinachomilikiwa na Kampuni ya Community Petroleum Ltd na klabu maarufu ya Meku's Bistro, iendelee kama kawaida na Kampuni ya Oryx Limited itoe mkataba wa miaka miwili. Msemaji wa Community Petroleum Ltd, inayoendesha shughuli zake katika mji wa Moshi ikiwamo eneo la kibiashara la Meku's, Emanuel Mlaki, amedai kuwa mpaka sasa hawaelewi ni kwanini mamlaka za serikali zinachelea kuchukua hatua za kusimamia utekelezaji wa amri hiyo ya mahakama.

Akizungumza na vyombo vya habari jana, Mlaki alidai kuwa licha ya kutolewa kwa amri hiyo, mawakili wao walikwenda Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Moshi na kufanya mapitio ya maombi kadhaa ikiwamo mapitio ya kuomba kuwaondoa watu walioingia katika eneo hilo kwasababu walikuwa wameingia kinyume na utaratibu.

Alidai kuwa na maombi waliyoyaomba yalikuwa ni 'mescilenious application no. 114' ya mwaka 2019 lakini pia walifungua maombi madogo, baada ya kuona kuna dalili fulani za vihatarishi kwa sababu ziko mali katika eneo hilo ambazo waliziachia na zinaharibika, hivyo ikabidi waiombe mahakama ndani ya maombi hayo kuitaka iamuru watu waondolewe na mahakama itoe zuio la muda la kuzuia watu wasiingie kwenye eneo hilo.

Aidha, alidai kuwa baada ya Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kujiridhisha kuhusu maombi yao na umuhimu wake, Mwenyekiti huyo James Silas, alitoa amri ya mahakama kuamuru watu wa Oryx na waliopo hapo wasifanye chochote katika eneo hilo. Amri hiyo ilitolewa Mei 6, 2019.

"Uko mkataba hapa (Deed of Settlement) ambao tuliingia baina ya Oryx na Community Petroleum Limited na mkataba huu ulisainiwa na pande zote zilizokuwa kwenye mkataba. Unakwenda kwenye eneo la mtu kumuondoa, viongozi wa serikali walitakiwa kuwapo, aidha mtendaji wa mtaa au mwenyekiti wa mtaa, hakuwapo.

"Kwa hiyo katika hali ya namna ile sisi haturidhishwi na lile tukio kwa sababu kampuni yetu iko kiuhalali, unavyoiona Meku's pale iko kiuhalali, unavyoiona Community Petroleum Limited iko kiuhalali."

Uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi kuagiza biashara ya kituo cha mafuta na klabu maarufu ya Meku's iendelee kawaida na kampuni ya Oryx Oil Ltd itoe mkataba wa miaka miwili umo katika uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza hilo alioutoa Mei 15, katika maombi yaliyowasilishwa na Kampuni ya Community Petroleum Ltd., inayoendesha biashara hizo.

Kampuni hiyo iliwasilisha maombi hayo dhidi ya Kampuni ya Oryx na Alphonce Mwacha, ikitaka Baraza hilo likazie hukumu iliyotokana na shauri namba 157/2017 lililosuluhishwa nje ya mahakama.




Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu (wa pili kushoto), akipokea moja kati ya mifuko 200 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 4.8 kutoka Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi, iliyotolewa msaada na benki hiyo, kwaajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo, juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Serengeti, Mhandisi Juma Hamsini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wahamasishwa kugombea nafasi za uongozi

**Na Paul William,** MOSHI.

VIJANA wa Chama cha Mapinduzi, wametakiwa kutumia fursa ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kutokana na serikali kuwa na imani nao.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, anaewakilisha vijana Mkoa wa Kilimanjaro, Zacharia Katikilo, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Alisema imefika wakati vijana hawapaswi kutumika kama daraja la kuwaingiza watu madarakani na badala yake wanapaswa kuwania nafasi mbalimbali za uongozi. "Vijana tumekuwa tukitumika katika kampuni mbalimbali kwa lengo la kukitetea chama, lakini kipindi hiki tunapaswa kutoka kifua mbele kwa

kugombea nafasi mbalimbali ndani ya serikali kwa kuwa vijana tukiamua

tunaweza," alisema Katikilo. Alisema, wapo baadhi ya vijana waliopewa nafasi mbalimbali za uongozi katika serikali hii na wamedhihirisha kwa vitendo kuwa wanawaweza na kuwataka wengine kuwaunga mkono kwa kugombea nafasi za uongozi uchaguzi utakapotangazwa.

Akizungumzia suala la vijana kutumika na baadhi ya wanasiasa kuvuruga amani ya nchi kwa kufanya maandaamano yasiyo na vibali, alisema imefika mahali vijana wanapaswa kukataa kutumika kama daraja kwa watu wengine na badaye kujiletea matatizo.

Katikilo alizungumzia pia suala la uundwaji wa vikundi mbalimbali vya vijana ili waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na halmashauri nchini bila ya riba na kudai kuwa serikali ilifanya hivyo ili kuhakikisha wanajikita katika shughuli za kimaendeleo na kujenga nchi yao.

"Nitumie fursa hii kuwakumbusha wakurugenzi wote wa halmashauri na majiji pamoja na manispaa kukumbuka umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya vijana kinamama na watu wenye ulemavu ambayo ni asilimia kumi ya mapato ya ndani kwani kufanya hivyo sio ombi bali ni matakwa ya serikali," alisema Katikilo.

# TRA yaelezwa changamoto za ulipaji kodi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro, imeagiza Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), mkoani hapo kuongeza ushirikiano na taasisi nyingine za serikali na vyombo vingine katika kupiga vita changamoto ya ukwepaji wa ulipaji wa kodi.

Pia uongozi wa mkoa huo umeagiza TRA kuweka mfumo mzuri wa udhibiti wa wakwepa kodi na wakwepakodi wachukuliwe hatua za kisheria huku vyombo vyote vya serikali kuagizwa kutoa ushirikiano katika kukusanya mapato ya serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema hayo katika uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Mlipakodi mkoani hapa kuwa serikali imetekeleza wajibu wake kwa kuongeza na kuboresha vitendea kazi pamoja ujenzi wa ofisi zenye hadhi na mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Alisema vitendo vya ukwepaji kodi vinachangia kukwamisha malengo na mipango ya maendeleo ya serikali hivyo vinapaswa kudhibitiwa.

"Imarisheni ukaguzi wa kumbukumbu za walipa kodi ili kutambua kodi iliyokwepwa, hakikisheni pia mnakusanya malimbikizo yote ya kodi ambayo hayajakusanywa ili kila mmoja atambue umuhimu wa kulipa kodi ni muhimu mfumo wa kodi ufahamike kwa wananchi wote."

"Maofisa wa TRA nawakumbusha hakikisheni mnachunguza na kuwatambua wafanyabiashara ambao hawalipi kodi na kuwaongeza kwenye wigo wa walipa kodi," alisema.

Aliwataka kuendelea kuboresha huduma wanazozitoa kwa wananchi katika utekelezaji wa majukumu na kutoa elimu zaidi.

Kaimu Meneja wa TRA mkoani Kilimanjaro, Rashid Herith, alisema makusanyo ya kodi yameongezeka kwa mwaka 2017/18 kwa kufanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.7 ikilinganishwa na mwaka 2016/17 makusanyo yalikuwa zaidi ya Sh. bilioni 1.5

Alisema wamekuwa wakikabiliwana changamoto mbalimbali katika ukusanyaji wa kodi ikiwamo baadhi ya wafanyabiashara kutokulipa kodi kama inavyostahili jambo ambalo limekuwa likiikosesha serikali mapato.

"Baadhi ya wafanyabiashara hawatoi risiti za mauzo na wengi hawalipi kodi kama inavyowapasa na hivyo kuikosesha serikali mapato yake," alisema.

Aidha, alisema wamejiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo ikiwamo kupambana na biashara haramu za magendo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wadau kuhusu sheria za kodi hususani zile za msingi.

"Tutaongeza juhudi ya kufuatilia na kukusanya malimbikizo ya kodi kutoa elimu ya kodi kwa wadau wetu, kupanua wigo wa kodi kwa kutembea mtaa hadi mtaa na pia tutaimarisha ukaguzi wa kumbukumbu za walipakodi mara kwa mara," alisema.

Mwenyekiti wa jumuia ya wafanyabiashra (TCCIA), mkoani hapa, Hillary Lyatuu, alisema mazingira ya mlipakodi mkoani hapa yameboreshwa kutokana na semina zianzofanywa na TRA Kilimanjaro katika wilaya zote.

"Hali ya kuimarisha mazingira ya uanzishwaji wa biashara inaendela kuwa nzuri ingawaje baadhi ya wafanyabiashara wamehamishia baishara zao sehemu nyingine na nchi nyingine na wengine kufunga, jambo hili lifanyiwe kazi kutafuta ufumbuzi," alisema.







Mtaalamu wa kilimo cha zabibu katika shamba la Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Mariamu Fissso (mwenye kofia katikati), akiwapa maelezo baadhi ya kinamama kutoka Wilaya ya Butiama na Musoma Mjini, walipotembelea shamba hilo, eneo la Zuzu, jijini Dodoma jana, kujifunza kilimo cha shamba darasa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Utafiti wabaini neema ya madini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UTAFITI uliofanywa na Korea kupitia mradi wa majaribio wa nchi za Afrika (AMGI) katika mkoa wa Ruvuma, umebaini baadhi ya maeneo kuwa na miamba yenye madini kama vile chuma na shamba kwenye tabaka la juu la ardhi.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu mkuu Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, alipokuwa akipokea ripoti ya utafiti huo jijini hapa.

Prof. Msanjila alisema pia taarifa zilizochukuliwa na ndege zinaonyesha kuwa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Ruvuma yana miamba yenye usumaku mkubwa, ambayo inaweza kuashiria uwepo wa madini ya chuma na mengine yanayoweza kuambatana na chuma kama vile metali mfano (Cu, Ni).

"Matokeo mengine kwenye taarifa zilizochukuliwa na ndege yanaonyesha uwapo wa miamba isiyo na usumaku kama miamba tabaka yaani yenye usumaku mdogo au isiyo kuwa na usumaku ambayo inaweza kuashiria uwapo wa madini yasiyokuwa na usumaku kwa mfano makaa ya mawe na urani," alisema Prof. Msanjila.

Aidha, alisema taarifa zilizochukuliwa na ndege zimeonyesha mipasuko kwenye ardhi ambayo ni muhimu kwenye kutafuta maji ardhi kwa kuwa ni chanzo kikubwa cha kupenyezaa maji na kuhifadhi chini ya ardhi.

"Mbali na maji, mipasuko hii inaweza kuwa mikondo ya kuhifadhi madini kitaalamu tunaita 'structurally controlled minerals'," alisema.

Katibu Mkuu pia alisema mbali na viashiria vya madini pia taarifa za jiolojia katika maeneo ya Ruvuma, kwenye mpaka wa Msumbuji na Tanzania pamoja na Tunduma kwenye mpaka wa Zambia zimeboreshwa kuwa za kisasa zaidi zikihusisha kutafuta uhusiano wa jiolojia kwenye maeneo ya mipaka.

Prof. msanjila aliishukuru serikali ya Korea kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kuendesha utafiti kupitia mradi wa AMGI.

Alisema ushirikano huo unatakiwa kuwa endelevu ili kuiwezesha Tanzania kufanya utafiti zaidi wa madini katika maeneo yote ya nchi.

"Utafiti huu ni muhimu sana tumekuwa tukisema nchi yetu ni tajiri wa madini lakini lazima tufanye utafi na kupitia utafiti kama huu ipo siku tunaweza kugundua uwapo wa madini ya Tanzanite katika mikoa mingine lakini pia hata almas katika eneo lingine tofauti na Shinyanga," alisema.

## Wataka utetezi haki za watoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuingilia kati suala la haki za watoto ili kuwanusuru na mimba zisizotarajiwa wakiwa katika umri mdogo.

Hayo yalielezwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, Fatuma Tofiq, wakati wa semina ya kuhusu mazingira hatarishi yanayowakabili vijana wadogo.

Taufiq alisema kuna kila sababu ya serikali kuingilia kati suala hilo kutokana na kuwa limekuwa tatizo kubwa kwa vijana wa rika hilo.

Alisema semina hiyo inapaswa kuwa changamoto kwa kila mmoja kujua atakwenda kuisaidiaje jamii huko wanakokwenda na kwamba kuna kila sababu ya kila mmoja kuhakikisha anapambana na kuwasaidia watoto.

Naye mwakilishi kutoka Shirika la Jukwaa la Utu wa Mtoto, Frolence Athio, alisema wako katika harakati za kutetea na kujuza haki za watoto na ustawi wa mtoto hususan wa kike.

Alisema kumekuwa na unyanyasaji wa watoto wa kike katika nyanja tofauti, jambo ambalo halikubaliki.

Kwa mujibu wa Athio, watoto wa kike wamekuwa wakilazimishwa kufanya tendo la kingono pasipo hiari yao, jambo ambalo wanalipinga vikali.

Katika semina hiyo ilioandaliwa na Shirika la Equality Now (CDF), washiriki wanajadili jinsi gani watoto wa kike wapewe haki yao kama ilivyo kwa watoto wa kiume.

Frolence, alisema lengo lao ni kuona wanafanikisha yale yaliyokusudiwa na shirika katika kutetea haki za mtoto hususani wa kike.

# Wapewa elimu ujasiriamali shamba la Pinda

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

ZAIDI ya kinamama 200 kutoka Mkoa wa Mara, wamewezeshwa mafunzo ya shamba darasa katika shamba la Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, lililoko eneo la Zuzu jijini hapa.

Mbunge wa Viti Maalumu kutoka Mkoa wa Mara, Agnes Marwa, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye eneo la shamba hilo alipopeleka kundi la kinamama kutoka Wilaya za Musoma na Butiama.

Marwa alisema kinamama hao wamewezeshwa masomo kuhusu elimu ya ujasiriamali na shamba darasa walipofika kujifunza kwenye shamba hilo.

Alisema alisema lengo kubwa la kupeleka kundi hilo kujifunza elimu hiyo ni kuwajengea uwezo wa kiuchumi ili kuinua uchumi wa familia zao.

Kwa mujibu wa Marwa, akiwa mbunge amefanikisha mafunzo hayo ikiwa ni ahadi yake aliyoitoa kuwapatia mafunzo ya ujasiliamali na ndani na nje ya mkoa wa huo.

Aidha alisema tayari baadhi ya kinamama kutoka Bunda, Musoma, Serengeti na Butiama wameshapatiwa mafunzo hayo kwa awamu kwenye shamba hilo ndani ya mwezi mmoja.

Hata hivyo, alisema mafunzo hayo ni endelevu na atahakikisha ndani ya wiki ijayo kinamama kutoka Tarime na Rorya wanafika kupatiwa mafunzo hayo ya shamba darasa.

Devotha Philipo, mmoja wa kinamama hao kutoka Musoma, alimshukuru Marwa kwa kuwawezesha safari hiyo ya mafunzo kwa vitendo ambayo yamewasaidia kujifunza aina mbalimbali za ufugaji.

Alisema katika shamba hilo wamejifunza ufugaji wa samaki, kuku, mbuzi, kondoo, bata na ng'ombe wa maziwa na nyama.

Naye Flora Tinga alisema elimu waliyowezeshwa kwenye shamba hilo wataipeleka kwa makundi mengine ambayo hayakupata fursa ya kufika hapo ili kujikwamua kiuchumi.

"Mimi ni diwani huko kwetu, nitahakikisha naitumia nafasi yangu kuwafikishia wengine elimu hii ya shamba darasa kwa makundi yote bila kubagua jinsia," alisema.





# Waziri aichongea ACT- Wazalendo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar asiye na Wizara Maalum, Said Soud, amemtaka Msajili wa Vyama vya Siasa kukichunguza chama cha ACT-Wazalendo ambacho kinaonekana viongozi wake kwenda kinyume cha Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kuhusisha imani za kidini.

Soud ambae pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima (AFP), aliyasema hayo wakati akichangia makadirio ya Ofisi wa Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema viongozi wa chama hicho kwa nyakati tofauti wameonekana wakifanya shughuli za kisiasa kwa kuhusisha imani za dini.

Kwa mujibu wa waziri huyo, sheria ya vyama vya siasa inakataza viongozi wa vyama kufanya kazi zao za kisiasa kwa kuashiria mwelekeo wa kidini.

"Mheshimiwa Spika, tunamwomba msajili wa vyama vya siasa nchini kukichunguza chama cha ACT-Wazalendo. Hivi karibuni viongozi wake walionekana wakifanya shughuli za kisiasa kwa kuingiza imani za kidini," alisema.

Soud alisema kama msajili atayapuuza matukio kama hayo, ni hatari na yanaweza kuligawa taifa katika misingi ya imani ya dini. "Mheshimiwa Spika, namwomba msajili wa vyama vya siasa ambaye majukumu yake yanafanya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukichunguza chama hicho na matukio hayo yanayohatarisha kuligawa taifa katika misingi ya imani za kidini," alisema.




Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Suleiman Ali Shihata wa Kijitoupele (kushoto) na Ahmada Yahya Abdulwakil wa kuteuliwa, wakipitia kurasa za gazeti la Nipashe wakati wa mapumziko nje ya ukumbi wa baraza hilo juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wataka chuo cha utumishi kuwezeshwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi, imetaka kuwezeshwa kwa Chuo cha Utumishi wa Umma Zanzibar (IPA) kufanya utafiti mbalimbali wa kitaalamu ili kuongeza mchango kwa serikali.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othman Said, alisema katika utafiti huo pia kufanyike ufuatiliaji wa wanafunzi ambao wamehitimu chuoni hapo ili kujua uwezo wao kiutendaji katika sekta wanazozihudumia.

Machano alisema kufanya hivyo kutasaidia chuo kujifanyia tathmini katika fani mbalimbali zinazotolewa kwa kila mwaka.

Mwenyekiti huyo alisema kamati hiyo imebaini kuwapo changamoto kubwa ya baadhi ya watumishi wa umma kushindwa kuzielewa kikamilifu kanuni za utumishi, hivyo kusababisha kushuka kwa nidhamu za utumishi katika maeneo ya kazi.

"Kushindwa kuzielewa kikamilifu kanuni za utumishi kumeathiri kwa kiasi kikubwa uwajibikaji kazini," alisema.

Aidha alisema Tume ya Utumishi Serikalini ina wajibu na jukumu la kusimamia watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na tume zingine za kiutumishi.

Kutokana na hali hiyo, alisema kamati inashauri kuendelea kusimamia watumishi wa serikali kupata haki zao na kuimarika maslahi yao.

Alisema kamati pia inashauri tume hiyo kusimamia kikamilifu na kuona kwamba watumishi wa serikali wanapatiwa fursa zaidi za kujiendeleza kielimu.

Machano alisema kamati hiyo imebaini kuwapo kwa changamoto kadhaa ambazo zinarudisha nyuma juhudi za watumishi wa ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumi wa Uchumi Zanzibar (ZAECA).

Pia alisema kamati imebaini wako baadhi ya watendaji wa ofisi za serikali na binafsi hawatekelezi majukumu yao ipasavyo, hivyo kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali na kurudisha nyuma harakati za kupambana na umasikini.

# Taasisi nyeti zalalamikiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Mamlaka ya Vitega uchumi na ile ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (Zura) ni miongoni mwa taasisi zilizolalamikiwa na Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ya Baraza la Wawakilishi kuwa hazijalipa ada ya ukaguzi wakati zina uwezo wa kulipa.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo katika kikao cha baraza hilo, Mjumbe wa Kamati hiyo, Rashid Makame Shamsi, alisema kutokana na matokeo ya uchunguzi huo, kamati imeiagiza ofisi ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali kutoza ada ya ukaguzi kuazia mwaka ujao wa fedha.

Alisema kamati hiyo inaamini kuwa kitendo cha ofisi hiyo ya mdhibiti kulipwa asilimia 10 pamoja na mamlaka hizo kulipa ada ya ukaguzi, kitaongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuimarisha huduma bora kwa jamii.

"Mheshimiwa Spika wakati PAC inapitia makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 ofisi hii imekadiriwa kukusanya Sh 56,915,000. Kamati yangu haikuridhika na kiwango hicho," alisema.

Alisema ofisi hiyo ndiyo taasisi inayokaguwa na kutoa dosari mbalimbali zinazojitokeza katika taasisi za umma kuhusiana na mapato na matumizi, hivyo wizara husika kuhakikisha inafuata taratibu zote za fedha kama sheria zinavyoeleza.

Mjumbe huyo akiwasilisha ripoti hiyo kwa niaba ya mwenyekiti wa kamati, alisema kamati inamtaka Waziri wa Fedha na Mipango kuhakikisha ripoti ya ukaguzi wa ofisi ya mdhibiti inawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Alisema kinyume cha kufanya hivyo itakuwa vigumu kamati yake kujadili na kupitisha bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 kutokana na kukosa uhalisia wa mapato na matumizi.



Soma UK. 15

**NIKKI WA PILI**


JUMAMOSI MEI 18, 2019

Nipashe

MWANGA WA JAMII

# BT

BURUDANI TELE



# NANDY

## ALIVYOMUIBUA UPYA RUGE

UK.14

## BASI SAWA



### Nandy alivyomuibua upya Ruge

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Faustina Charles Mfinanga, maarufu kama Nandy ameibua mjadala upya wa uhusiano wake na aliyekuwa Mkurugenzi wa vipindi katika kituo cha redio cha Clouds, marehemu Ruge Mutahaba.
Mapema wiki hii akizungumza na kituo kimoja cha televisheni ya mtandaoni, Nandy alisema kuwa walipanga kufunga ndoa Machi mwaka huu.
"Hatukupenda mahusiano yetu yaendeshwe na mitandao kwa sababu najua ingekuwa balaa na ndio maana ikawa siri," alisema.
Akielezea alivyoanza mahusiano hayo na marehemu Ruge mwanadada huyo alisema alikuwa akipenda kumshirikisha mawazo yake hata mambo yake binafsi.
"Tuliingia kwenye penzi zito na ilikuwa tufunge ndoa mwezi Machi mwaka huu," alisema Nandy.



### Mr T Touchez: Da! Rayvanny ni noma sana

MTAYARISHAJI wa muziki wa bongofleva, Mr. T Touchez, amesema alichokifanya Rayvanny kwa kumzawadia gari produza wake ni funzo kubwa kwa wasanii wengine.
Mapema wiki hii Rayvanny alimzawadia gari produza wake, S2kizzy wakati akiazimisha siku yake ya kuzaliwa.
Baada ya tukio hili, T Touches alisema alimpigia simu Rayvanny kumpongeza na kuwambia alichokifanya ni kitu kizuri zaidi.
"Nilimpigia Rayvanny nikamwambia umeonesha utofauti na utawafunza wasanii wengi kwamba hii kitu inatakiwa mwisho wa siku iwe hivi, kwa sababu hawa watu hawapati kitu na kama huwezi kujiongeza.
"Huwezi kufanya show huwezi kufanya kitu kingine mwisho wa siku unajikuta umeshatengeneza hit, lakini huwezi kupata unachohitaji kwenye maisha," Touchez.



## CHUCHU amchana Ray siku ya 'besidei'

NYOTA wa kike wa Bongo muvi, Chuchu Hansy, amefunguka kuhusu mzazi mwenzake Vicent Kigosi maarufu kama Ray, kuwa baada ya kupata mtoto wao aitwaye Jaden, alijiona baba mpaka wa watoto waliokomaa.
Chuchu ameliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram wakati akimtakia heri ya siku ya kuzaliwa mzazi mwenzake huyo akiwa ametimiza umri wa miaka 39 mapema wiki hii.
Chuchu aliandika; "Happy Birthday baba @jadenthegreatest baba mwenye jeuri zako baada ya kupata mtoto ukajiona baba mpaka kwa watoto wakubwa waliokomaa."
Hata hivyo, mrembo huyo alisema kuwa hana tatizo na Ray na kusisitiza hivi na aliandika tena, "No matter what nakutakia Happy Birthday Mungu azidi kukuweka inshaalah uje mleane na mwanao, sina zawadi, kubwa zawadi yangu ni @ jadenthegreatest na natumai ni zawadi ya milele na yenye historia kwako."

## INSTA-TWITTER





**Watu** wa nyimbo mpya naombeni utulivu tafadhali- **Ben Pol**



**Ukiona** shida zinazidi ujue neema zinakaribia, kwa hiyo tujifunze kutokukata tamaa mhenga mmoja aliniambia haya- **Nandy**



## Ferooz arudi kwenye game na G Nako

MSANII wa bongofleva aliyewahi kukimbiza mno na songi lake la Starehe, Ferooz amerudi upya na safari hii yupo na songi jipya alilolipa jina la 'Excellent'.
Ferouz ambaye alikuwa kwenye kundi la Daz Nunda amekuja na wimbo huku akimshirikisha rapa kutoka Arusha G Nako.
Songi hilo Ferooz aliliachia mapema wiki hii na kuonekana kupokelewa vizuri na mashabiki wake na limeaanza kupigwa kwenye mitandao ya kijamii.
Mashabiki wake wengi walilipokea songi hilo katika mitando ya kijamii walionekana kukubali na hivyo huo unaweza kuwa mguu mzuri wa kuridi kwenye fani kwa mkongwe huyo Farooz, likiwa limepigwa na produza Mocco Genius.



@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...

# Nikki wa Pili yamkuta, atolewa povu la kufa mtu



NYOTA wa muziki wa Hip Hop, Nikki wa Pili, amejikuta katika wakati mgumu baada ya kutoa maoni yake tofauti na kitabu cha Biblia juu ya uumbaji wa mwanamke.
Nikki wa Pili alitoa maoni yake kwenye mitandao ya kijamii kwa kusema kuwa sio kweli mwanamume alikuwa wa kwanza kuumbwa na Mungu kama Biblia inavyoeleza, bali mfumo wa zamani ulikuwa mfumo dume na Biblia iliandikwa na wanaume.
"Stori inayosema Mungu alimuumba kwanza mwanamume, alafu baadae akaja kumuumba mwanamke kutoka mbavu zake, nadhani iko hivyo kwa sababu imeandikwa na mwanamume na iliandikwa kipindi ambacho jamii zilikua nyuma sana katika haki za kijinsia, ni Stori ya kimfumo dume," aliandika Nikki wa Pili.
Maoni hayo yalipokelewa tofauti na mashabiki wake pamoja na wasanii wenzake akiwemo Billnass ambaye alimwambia kuwa amefikia hatua ya kukosoa Biblia kisa kuoa mwanamke, huku wengine wakimuita limbukeni.

## BODA 2 BODA



# Daz Baba aja na Karibuni Tanzania

ALIYEKUWA nyota wa kundi la Daznunda, Daz Baba, amerudi kivingine na kuachia video ya wimbo wake mpya 'Karibuni Tanzania'.
Wimbo na video hiyo ameitengeneza maalumu kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii nchini.
Daz Baba ameachia video hiyo baada ya kukaa kimya kwa muda mrefu na sasa anaonekana kugeukia zaidi kwenye utalii.
Video hivyo imefanyika na muongozaji Chidy Bwax pamoja na Jacktan Kibiki, huku audio ikiwa imefanywa na produza Roxer.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Pale** unapomuona mtu anayekudai kakufuata na ulikua humpokelei simu-**Timbulo.**



**Kwani** 'Next Week' tukiachia ngoma nyingine kuna ubaya?-**Nay wa Mitego.**



**Naiusia** nafsi yangu na nyinyi pia. Tumwogope Mwenyezi Mungu popote pale tulipo-**Ali Kiba.**

# Vijimambo

1. Haya mambo ya kidigitali yatabaki kuwa juu - Shirima, Morogoro.
2. Wenzetu panya wanategua mabomu, sisi wanapiga picha - Seur Abel, Arusha.
3. Kamera yangu mbovu, na pesa ya matengenezo sina - Haji, Zenji.
4. Huu mtambo lazima utoe picha za maana - Mama Nah, Manzese DSM.
5. Bingooo! Hii narusha instagram kwanza sasa hivi - Augustino S. Doe, Arusha.
6. Mmh, sijampata vizuri huyu boya aliyekatiza mbele ya kamera - Augustino S. Doe, Arusha.
7. Sijui napatia au nakosea, haya mambo ya binadamu matata sana - Juma Uledi, Zenji.
8. Ngoja kwanza niutesti mtambo kabla sijaanza kazi rasmi - Njuma Idi, Mikocheni DSM.
9. Hapa lazima nipate picha kali ya mwaka - Athanas Migomba, Mabibo Mwisho DSM.
10. Watu bwana, badala ya kunipa ndizi wananihangaisha na huu mtambo! - Juma Uledi, Zenji.
11. Ngoja sasa niifungulie dunia namna mpya ya kupiga picha - Sakina Mande, Muheza Tanga.
12. Komaa mzee baba, mdogo mdogo utatoa picha bomba - Beneali Mousea Beneali, Migombani Zenji.
13. Mnashangaa nini? Si mlisema binadamu wa kwanza tulikua sisi? - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Picha napiga vizuri tu, wanazisifia, tatizo malipo hawanipi - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
15. Yees! Huu mtambo nimeukubali mia kwa mia. Acha sasa nionyeshe maajabu - Lina Monday, Korogwe.
16. Hii naikorokochoa mpaka nione walikoficha ndizi - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
17. Acha tu nibahatishe kama nitaweza, maana chombo cha kizungu hiki - Tausi Monday, Old Korogwe Tanga.
18. Haya sasa, fanya vitu vyako ulimwengu ukutambue ukuweke kwenye rekodi - Theophile Lema, Mbezi Louis DSM.
19. Mnanishangaa mimi kupiga picha, je mngemuona babu yangu akinipiga picha hii? - Tulo Hoza, Mjasana Tanga.
20. Jamani eeh, hii kamera ni ya picha za 'black and white', msije mkanipora bureee! - Njuma Iddi, Mikocheni DSM.
21. Huu ndio ulimwengu wa kidigitali kwa kila kiumbe. Usizubae mzee baba! - Manka Ndemfoo, Kimara Mwisho DSM.

**SMS Bomba ya Leo:**
Mnanishangaa mimi kupiga picha, je mngemuona babu yangu akinipiga picha hii? - Tulo Hoza, Mjasana Tanga.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0682 808 694**



## Najua Kuoa
## Mapenzi ni ridhaa, hayalazimishwi

**Na Adam Fungamwango**

MAPENZI ni ridhaa ya watu wawili, mwanaume na mwanamke wanapoamua kuanzisha uhusiano.

Si mwanaume au mwanamke anayelazimishwa kumpenda mwenzake. Kinachotakiwa hapo ni mwanaume tu, kumuonyesha mwenzake na kumshawishi kuwa anamhitaji. Kinachobaki hapo ni ridhaa ya mwanamke.

Na hata wanapoishi pamoja kwenye ndoa, bado ridhaa inakuwa pale pale na mmoja anapochoka kwa sababu zozote zile, ziwe za kweli au za kushawishiwa, ndoa huyumba, tafrani inazuka ndani na hatimaye inavunjika. Mapenzi siku zote hayalazimishwi, ndiyo maana hali inapokuwa ngumu sana, watu huamua kutengana.

Hili limeonekana kwenye filamu ya 'Najua Kuoa' Ni filamu ambayo inatoa funzo kwa wenye ndoa na ambao bado hajaingia kwenye taasisi hiyo. Imechezwa na Riyama Ally, hayati Mzee Majuto, Ally Nogi na wengineo.

Awali, maisha ya Riyama na mumewe Ally Nogi yalikuwa ya raha sana. Waliishi kwa amani na utulivu.

Kuna kijana mmoja anaitwa Hamza, aliyetoka mjini kuja kijijini kumsalimia mama yake.

Huyu ndiye aliyezua balaa. Riyama baada ya kumuona kijana huyo, akili ikamruka, akazuzuka.

Penzi likahama kwa mumewe na kuhamia kwa kijana huyo. Usiku akawa halali anamuota Hamza.

Riyama anamtumia kijana muuza genge ambako ndiko alikomuona, ili amuelezee Hamza alivyokufa juu yake. Kwanza Hamza anasita kuingia kwenye uhusiano huo, lakini kutokana na kushawishiwa pesa na mwanamke, aliingia mzima mzima.

Bila kujali nafasi ya mumewe. Bila kujali ni mke wa mtu, Riyama alijiingiza kwenye mapenzi na kijana huyo, ikawa si siri tena kwenye kijiji hicho.

Kibaya zaidi mumewe akapata habari. Ally Nogi licha ya kufahamu, lakini hakuchukua uamuzi wowote. Mke akawa anazidisha vitimbi ili aachwe, lakini mume akikaza uzi na kudai kuwa yeye anajua kuoa na si kuacha licha ya kuwafumania mara kadhaa.

Visa vyote anavyofanyiwa, lakini wapi, mzee kakomaa tu na mke wake. Riyama akaona ampikie mboga ya jongoo ili amkere apate talaka yake aishi na kibenteni chake kwa raha mustarehe.

Baada kukuta kumbe mboga yenyewe iliyoungwa vizuri ni jongoo, alikasirika akaamua kuandika talaka. Lakini kabla ya kumpa akaichoma moto. Riyama akaamua kwenda kwa mganga ili kumuua mumewe. Ally Nogi anafariki dunia na muda mfupi tu, Riyama anaolewa na Hamza.

Ndugu za marehemu hawakukubali. Nao wakaenda kwa mganga kulipiza kisasi. Hamza akapooza mwili huku Riyama akigeuka kuwa chini. Ally Nogi tangu mwanzo alipoona visa hadi visa, angeamua kuachana naye haya yote yasingetokea. Alilazimisha kuendelea kuishi na mwanamke ambaye moyoni mwake hakuwa na ridhaa kwake tena.



# Pombe
## ZIMEMMALIZA BRITNEY SPEARS

**LOS ANGELES, Marekani**

MENEJA wa muda mrefu wa Britney Spears, Larry Rudolph, amedai kwamba muimbaji huyo wa Pop kamwe hataweza tena kutumbuiza jukwaani kutokana na matatizo ya kiafya.

Britney (pichani)anasumbuliwa na matatizo ya kiafya yanayotokana na unywaji wa pombe kupita kiasi.

Muimbaji huyo mwenye umri wa miaka 37, alilazimika kuahirisha maandalizi ya ziara yake ya kimuziki aliyoipa jina la 'Britney: Domination Las Vegas' baada ya kuendelea kutibiwa kwenye rehap.

Nyota huyo awali alisitisha ziara hiyo ya kimuziki mapema mwaka huu, lakini kwa mujibu wa meneja wake huyo wa zamani, Britney hataweza tena kurudi jukwaani.

Larry mwenye umri wa miaka 55, ameiambia TMZ: "Kwa mtu ninayemjua na niliyefanya kazi kwa muda mrefu pamoja na watu wake wote wa karibu wanaona kwamba Britney hataweza tena kurudi jukwaani.

"Siyo tu hataweza kurudi hivi karibuni, lakini naona kwamba hakuna uwezekano wa yeye kurudi tena jukwaani kwa siku za usoni."

Meneja huyo alikuwa na Britney kwa zaidi ya miaka 20, akianza naye kuanzia mwaka 1998.

Onyesho la muziki la Britney awali lilipangwa kufanyika Februari 13 mwaka huu, huku alikuwa akitarajia kufanya shoo 32 kuanzia Agosti 17, lakini ikahirishwa hadi Januari 4 mwaka huu.

Hata hivyo, mapema mwaka huu tena ziara yake hiyo ikaahirishwa kutokana na hali yake kutoimarika na kurudishwa tena rehab ambako anatibiwa kutokana na matatizo ya kutumia pombe kupita kiasi.

Mkali huyo wa kibao cha 'Baby One More Time' amekuwa kwenye utumiaji wa pombe kupita kiasi hali iliyoathiri kwa kiwango kikubwa afya yake na sasa anaendelea na matibabu kwenye rehab.

Britney alipoingia kwenye muziki aliliteka vilivyo soko na kuonekana kwamba angekuja kusumbua zaidi kwa siku za usoni.

Lakini sasa ni miaka zaidi ya 20, muimbaji huyo anaelekea shimoni na ni wazi kwamba uwezekano wa kuinuka tena ni mdogo.

Kipaji chake kilianzia kwenye Klabu ya The Mickey Mouse, na Britney alionekana kuwa nyota nzuri zaidi kwa muziki wa Pop na akapewa jina la Princess of Pop, baada ya albamu zake mbili za kwanza za 'Baby One More Time (1999) and Oops!... I Did It Again (2000).

Albamu hizo mbili zilitawala chati nyingi duniani na kumfanya kuwa mwanamuziki mwenye mafanikio makubwa zaidi katika umri wake mdogo.

Februari mwaka 2007, mshindi huyo wa tuzo kadhaa alilazimika kuanza matibabu kwenye rehab kutokana na utumiaji wa pombe kupita kiasi.

Britney na mume wake wa zamani Kevin Federline mwenye umri wa miaka 41 ambaye alikuwa dansa wake, walioana mwaka 2004 na wakaachana mwaka 2007 na wana watoto wawili wa kiume, Sean mwenye miaka 13 na Jayden mwenye miaka 12.

Mwisho.

# Kim Kardashian awa saidia wafungwa 17

MWANAMITINDO wa Marekani, Kim Kardashian, hivi karibuni amesaidia wafungwa 17 kuachiwa huru kufuatia kampeni yake ya '90 DAYS OF FREEDOM" iliyozinduliwa rasmi na wanasheria wake Brittany Barnett ambaye anashirikiana nae katika kuendesha kampeni hiyo.

Kardashian ambaye ameungana na Barnett pamoja na MiAngel Cody wameamua kufanya kampeni hiyo mara baada Rais wa Marekani, Donald Trump, kusaini hatua ya kwanza ya sheria inayoruhusu baadhi ya watu waliofungwa kwa tuhuma za dawa za kulevya kuomba kupunguziwa adhabu.

Kufuatia hatua hiyo kwa sasa Kim Kardashian amekuwa akipokea simu nyingi kwa watu mbalimbali wakihitaji msaada wa ndugu zao waliopo jela ili wapatiwe msaada wa kuachiwa uhuru.

Kim alianza rasmi kujihusisha na kampeni hiyo mara baada ya kumtembelea Rais, Trump Ikulu yake mwaka jana kumtetea, Alice Marie Johnson mwenye umri wa miaka 63 kutoka Alabama ambaye alifungwa kifungo cha maisha kwa kesi ya matumizi ya madawa ya kulevya na sasa ni mmoja ya waliopokea msaada wa kuachiwa huru baada ya kutumikia kifungo jela kwa miaka 12.





## J Lo kumrithisha kipaji binti yake

JENNIFER Lopez anapanga kumuingiza mtoto wake wa kike mwenye umri wa miaka 11 kwenye tasnia ya muziki.

Kwa kuanza binti yake huyo aliimba vizuri wimbo wa Alicia Keys na sasa mkali huyo wa kibao cha 'Get Right' anataka mwanae huyo aingie mazima kwenye tasnia hiyo.

Binti huyo aliimba vizuri wimbo wa Alicia wa 'If I Ain't Got You' alioutoa mwaka 2003 ,katika tamasha la mama yake.

"Ameimba vizuri wimbo wa Alicia Keys," alisema J.Lo. "Alikuwa vizuri na nilipendana anarithi kipaji changu," aliandika J Lo kwenye ukurasa wake wa Instagram.

J Lo alizaa mapacha na mwanamuziki, Marc Anthony baada ya kudumu kwa kipindi kifupi kweye mapenzi na Ben Affleck na sasa amechumbiwa na Alex Rodriguez.

## Picha yamuingiza matatizoni Ariana Grande


NYOTA wa muziki wa Pop na R&B, Ariana Grande, ameingia matatani kuhusu haki miliki baada ya kuposti picha kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Ariana aliingia kwenye matatizo hayo baada ya kuposti picha hiyo ambayo hakuilipia kutoka kwenye mtandao wa kijamii.

Posti yake hiyo ilitembelewa na watu milioni 3 wali 'like' kabla ya yeye mwenyewe kuifuta baadae.

Mpigapicha, Robert Barbera, alidai kwamba, Ariana hakuomba ruhusa kutoka kwake katika picha zake mbili alizompiga ambazo zina hatimiliki yake.

Na sasa Barbera anataka alipwe dola 25,000 (sawa na zaidi ya Sh. Milioni 50) kwa kutumia picha hiyo bila ruhusu.






## Mkali wa muvi za James Bond aumia mguu akipiga picha

DANIEL Craig ambaye kwa sasa anaigiza muvi za James Bond, aliumia kifundo cha mguu wakati akipiga picha kwenye muvi mpya.

Mkali huyo wa mapigano mwenye umri wa miaka 51 alikumbwa na kisanga hicho wakati akiigiza muvi mpya ya James Bond huko nchini Jamaica.

Gazeti la The Sun limeripiti kwamba Daniel wakati anapiga picha katika moja ya matukio ya muvi hiyo nchini Jamaica aliangia na kuumia kifundo cha mguu.

"Alionekana kuumia na baadaye iligundulika kwamba aliumia kifundo cha mguu. Na hivyo sasa anauguz kwanza majeruhi yake kabla ya kurudi tena kumalizia kuigiza muvi hiyo.

SAFU



Na John Juma
0716217615

Mionzi ya Sheria

## Wajenzi mabondeni, nini haki na wajibu wako kisheria?

MVUA zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali na atahri zake zimeonekana. Mionzi ya Sheria leo inajikita kujibu swali la msingi hapo juu. Ni vyema kuanza kuyajua makundi ya ardhi yanayotambulika kisheria.

Kwa ajili ya usimamizi na utawala wa ardhi, Sheria ya Ardhi nchini Tanzania, (The Land Act Cap. 113), ya mwaka 1999 inaigawa ardhi katika makundi matatu: Ardhi ya jumla; Ardhi ya Vijiji'; na Ardhi ya Hifadhi. Ardhi ya jumla, ni ambayo haiangukii miliki ya vijiji au hifadhi. Hii ni miongoni mwa ardhi inayosimamiwa na Sheria ya Ardhi ya 1999 na kiutendaji inasimamiwa moja kwa moja na serikali.

Ardhi ya Vijiji: Ni maeneo yaliyo ndani ya kijiji kinachotambulika kisheria na inasimamiwa na serikali ya vijiji. Hii ni pamoja na ardhi iliyo ndani ya mipaka ya vijiji, ambayo imesajiliwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Local Government Act) 1982; 'ardhi iliyo chini ya vijiji vilivyoanzishwa chini ya Sheria ya Makazi (Village Settlement Act) 1965'.

Pia, kuna ardhi iliyotengwa kama kijiji, kwa lengo maalum na kuwekewa mipaka kwa kufuata sheria zilizowekwa; ardhi yoyote ambayo mipaka yake imekubaliwa na Serikali ya Vijiji husika, hasa pale ardhi hiyo ilikuwa na mgogoro.

Pia, katika kundi hilo la wamiliki ardhi, wanaingia wanakijiji wanaoimiliki kwa muda wa miaka 12 au zaidi kabla ya kupitishwa Sheria mpya ya Ardhi mwaka 1999'.

Ardhi ya Hifadhi: Ni iliyotengwa kwa madhumuni maalum. Hii ni pamoja na Hifadhi ya Misitu inayotambulika kisheria; mbuga za wanyamapori; hifadhi za majini, ikihusisha bahari, mito, mabwawa makubwa na maziwa'; 'hifadhi za barabara; maeneo ya wazi ya kupumzikia, burudani, michezo na starehe; na, ardhi hatari.

Mifano ya hai ni mabondeni, penye miteremko mikali, kingo za mto, maziwa na bahari, sehemu zilizotengwa kutupa taka, mito na miamba baharini.

Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, kupitia Kifungu cha 6(1) (d)] na Sheria ya Ardhi ya Vijiji; Kifungu cha 6(1)-(11)], zote kwa ujumla wake zina tamko kuhusu ardhi hatari.

Inaitafsiri: "Ardhi Hatari" ni ambayo si salama kwa maisha ya ama binadamu au viumbe vingine, au utumiaji wake unaleta uharibifu wa mazingira."

Kabla ya haijatangazwa kuwa 'Ardhi Hatari" kama Sheria Kuu ya Ardhi inabainisha, wanaomiliki ardhi hiyo wapewe nafasi kutoa maelezo, yatakayozingatiwa katika kufikia maamuzi.

Baada ya uamuzi wa kuitangaza sehemu yoyote ya ardhi kuwa 'Ardhi Hatari, wamiliki wote kisheria hulipwa fidia kulingana na sheria inavyoelekeza kwa wakati huo, pia inatangazwa katika Gazeti la Serikali, ili kuufahamisha umma wa Watanzania.

**TAMKO LA SHERIA RASMI**

Kifungu cha 57(1) cha Sheria elekezi ya mazingira kinasema, hakuna atakayeruhusiwa kufanya shughuli za kibinadamu za kudumu ndani ya mita 60, ambazo kwa asili yake zinaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira au utunzaji bahari au kingo za mto, bwawa, na miamba ya asili ya ziwa.

Hiyo ni sawa na kusema, serikali kwa kupitia mamlaka zake zenye dhamana, moja kwa moja, inawajibika kuhakikisha raia wake wanaendeleza makazi na ikiwemo kuendesha shughuli zao za kila siku katika mahali salama na halali kwa mlengwa huo. Sheria ya Usimamizi wa Mazingiraya Mwaka 2004), inatamka kuwa Waziri mwenye dhamana, anaweza kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo husika.

Hivyo basi, kwa ujumla wake kinachosisitizwa ni kwamba mtu ataruhusiwa kuendeleza makazi katika ardhi isiyokuwa hatarishi tu na siyo kinyume na mazingira hayo. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Mwaka, 1999.

Pia, Sheria ya Mipango Miji, inatamka mtu hataruhusiwa kuliendeleza eneo lolote lililopimwa kwa mujibu wa sheria, bila ya kwanza kupatiwa kibali maalum toka kwa mamlaka husika, kwa kuzingatia masharti yanayoambatana na kibali husika.

Ni utaratibu unaojitokeza katika Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

**MUHIMU**

Sheria inaenda mbali zaidi kwa kutoa mwanya kwa raia kuiomba mahakama kutoa "amri ya hafueni" pale atakapotakuwa na mamlaka yenye dhamana kuondoka katika eneo, kutokana na sababu za kisheria.

Haki hiyo ni imo chini ya Sheria Elekezi ya Mmasuala ya Ardhi.

Angalizo ni kwamba, kwa Kifungu chake kidogo cha 9 (a)-(c): Maombi haya ya kuiomba Mahakama kutoa 'amri ya afuheni' kamwe hayatachukuliwa kwamba mwombaji hana haki ya msingi juu ya eneo lake.

Mfano hai, rejea hatua ya Mahakama Kuu katika mwaka 2016, kukubali kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi Ombi la Wakazi wa Mabonde ya Kinondoni, waliopipinga hatua ya serikali kuvunja nyumba zao kwa lazima na kuwataka kuhama bila ya fidia.

**HITIMISHO**

Kimsingi, fidia ya ardhi ni stahili ambayo mmiliki wake anapaswa kulipwa, pale tu ardhi yake inapotwaliwa. Yaweza kuwa kwa matumizi ya serikali, binafsi au hata kwa ya aina nyingine yoyote ile, ambayo kwa tafsiri itakuwa ni 'kwa manufaa ya umma.'

Kwa kuwa basi, mmiliki halali wa ardhi ndiye pekee kisheria ana haki ya kudai fidia, anaweza kuwa mtu binafsi, kampuni, shirika au taasisi ya aina yoyote, , kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji. Atakayestahili fidia, anatajwa ni yule tu ambaye hajaendeleza makazi au kufanya ujenzi katika eneo la wazi lililotengwa kwa ajili ya shughuli za kijamii na aliyeendeleza makazi kwa kuzingatia vigezo na masharti yanayoambatanishwa katika hatimiliki ya ardhi aliyopatiwa na mamlaka yenye dhamana.

Hivyo basi, kutokana na hicho kilichotangulia kuelezewa, kwa wale wote waliojenga katika maeneo yasiyostahili kisheria watakuwa hawana haki yoyote wala shauri la madai msingi, dhidi ya serikali. Sheria Elekezi ya Masuala ya Ardhi, Kinamtaka mnunuzi wa ardhi kuwa makini sana ya kujiridhisha, au maarufu (buyer beware).

Pia, kwa wapangaji, katika nyumba au majengo ya biashara, ambayo ujenzi wake haukuzingatia vigezo na masharti, nao wako hatarini kupoteza haki zao. Naomba kuwasilisha!



Reubeni Lumbagala

Kalamu ya Mwalimu

## Kifo cha Dk. Mengi kimeacha pengo katika sekta ya elimu

TAREHE 2 Mei, 2019, nchi yetu ilipata pigo kubwa la kuondokewa na Mtanzania mzalendo, mdau wa maendeleo na mwekezaji mkubwa Dk. Reginald Abraham Mengi, kilichotokea huko Dubai.

Hakika ilikuwa ni simanzi kubwa kufuatia mchango mkubwa aliyoutoa Dk. Mengi katika maendeoleo ya nyanja mbalimbali kama vile elimu, afya, michezo, mazingira na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Hakika mchango wake hautaweza kusahaulika kutokana na kugusa maisha ya Watanzania wengi na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Leo niunagane na waliokwishasema, kuangazia mchango wa marehemu Dk. Mengi kwa uchache katika sekta ya elimu, ambayo ni sekta muhimu kwa ustawi wa maisha ya wananchi na ukuaji maendeleo ya nchi.

Yapo mengi ambayo Dk. Mengi, aliyafanya enzi ya uhai wake, katika kusaidia wanafunzi moja kwa moja na kusaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Pindi marehemu Dk. Mengi, alipokuwa akialikwa katika mahafali ya shule mbalimbali kama mgeni wa rasmi, alikuwa akitoa nasaha nzuri kwa wanafunzi kuhusu umuhimu wa kusoma kwa bidii ili kufanikiwa katika maisha yao.

Sambamba na hilo, aliahidi kutoa zawadi ya fedha kwa wanafunzi watakaopata daraja la kwanza. Mara nyingi aliahidi kutoa fedha kutoka Sh. milioni moja kwa kila mwanafunzi atakayefaulu kiwango cha daraja la kwanza katika mitihani ya taifa.

Pia, katika mahafali ya 24 ya Kidato cha Sita katika Shule ya Wasichana ya Ashira, Dk. Mengi aliahidi kutoa Sh. milioni moja kwa kila mwanafunzi atakayefaulu mitihani yake ya kitaifa kwa kupata daraja A.

Dk. Mengi alitimiza ndoto za wanafunzi wengi kupata elimu kwa kugharamia ada na mahitaji yao muhimu ya shule. Mathalani, wilayani Simanjiro, aliwasomesha wanafunzi wengi wa jamii ya Kimasai kupata elimu bora.

Vijana na watoto wengi wa Tanzania, wameweza kupata elimu kupitia ufadhili uliokuwa ukitolewa na Dk. Mengi. Msaada huo umewezesha wanufaika wa ufadhili kujitegemea, baada ya kuhitimu masomo yao na kuwa msaada kwa familia, jamii na nchi kwa jumla.

Watu wengi, wakiwamo wanafunzi wenye mahitaji, walikuwa wakinufaika na misaada mahsusi kwa watu wenye mahitaji maalum.

Kwa mfano, Mathalani, mafuta kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa ngozi na baiskeli, ili ziwasaidie kufika shule na kupata elimu. Misaada hiyo iliongeza ari kubwa kwa watu wenye ulemavu kusoma kwa bidii na kujiona wanathaminiwa ndani ya jamii.

Daima Dk. Mengi alikuwa kinyume na dhana potofu kuwa watu wenye ulemavu hawawezi kufanya vizuri katika masomo.

Aliwajengea imani ya kujiamini na kujikubali kuwa wao sio watu walemavu, bali ni watu wenye ulemavu na wana uwezo sawa na hata zaidi ya wasio na ulemavu, katika kufikia malengo makubwa kwa maendeleo.

Katika kuhakikisha miundombinu ya kutolea elimu inakuwa bora, Dk. Mengi alichangia rasilimali fedha, ili isaidie kuboresha elimu. Alikuwa mdau mkubwa wa kuchangia madawati.

Dk. Mengi hafurahishwa na changamoto ya wanafunzi kukaa chini shuleni. Hali hiyo, ilimfanya kuchangia fedha nyingi kusaidia upatikanaji madawati.

Nakumbuka aliwahi kuchangia Sh. milioni 70, kwa ajili ya kusaidia madawati ya shule za wilaya za Handeni mkoani Tanga na Bagamoyo Pwani. Kila wilaya ilipata mgawo wa Sh. milioni 35, iiyowezesha kupatikana madawati 1,000 kwa ajili ya shule za msingi na sekondari.

Aidha, alichangia Sh. milioni 151 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira.

Dk. Mengi aliahidi kutoa Sh. bilioni moja, kusaidia ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Sekondari Jumuishi ya Mtakatifu Pamakio.

Kutokana na mchango wake huo, Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, Mhashamu Isaac Amani, alimtunuku tuzo ya Msamaria Mwema, kutokana na kusaidia watu wenye mahitaji maalum

Katika harambee ya kuchangia ujenzi, Dk. Mengi alisema: "Leo naona hawa wenzetu waliotoka nje wameahidi kutoa misaada na sasa hapa ni nyumbani na mimi naahidi kutoa mchango kidogo, Baba Askofu Amani kwa Sh.bilioni moja."

Baada ya kutamka ahadi hiyo, watu walimshangilia, ghafla Mzee Mengi alisema "Naomba msinishangilie, tumshukuru Mungu kwa sababu mimi ni bomba tu, anayeweka maji ni Mungu na siyo mimi. Mwenyezi Mungu ndiye anayesema peleka maji pale kwa watu wenye kiu. Kwahiyo na haya maji Mungu akipenda hayatakauka."

Ni muhimu Watanzania wote kujifunza kwa marehemu Dk. Mengi, alikuwa na moyo wa kizalendo kusaidia wenye mahitaji, ili waweze kufikia ndoto, maono na malengo waliyojiwekea. Hakika kifo cha Dk. Mengi kimeitikisa sekta ya elimu.

● **Reubeni Lumbagala ni mwalimu kwa taaluma kutoka Shule ya Sekondari Mlali, iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Anapatikana kwa simu: Maoni: (+255) 0764 666349.**

# ASASI YA PLAN INAVYOW
# KISARAWE KUTOKA ZAM

## ■Bweni, mikakati mipya yabadili ufaulu
## ■Vyoo vya kihistoria, hedhi si tatizo tena
## ■DC, kinamama 'walioula' mifano ya kuigwa

**Na Zuwena Shame,** KISARAWE

**JANA katika jarida maalum gazetini (BUFE), ilielezea jitihada za asasi ya Plan International, kwa kushirikiana na serikali wilayani Kibaha, walivyofungua milango ya maendeleo kwa wakazi. Endelea na namna ilivyofungua milango ya kuwakomboa wasichana dhidi ya mimba na usalama wa maisha yao wilayani, Kisarawe, katika mkoa huohuo wa Pwani. Fuatilia ushuhuda huo;**

HAKI ya elimu ni muhimu sana kwa kila mtoto, kama zilivyo haki zingine muhimu kama vile malazi, chakula, kuishi, kulindwa na kusikilizwa.

Pia mtoto wa kike ana haki ya kupewa elimu sawa na mwenzake wa kiume, katika mtazamo ukimuelimisha mtoto wa kike, basi ni jamiim nzima imeelimishwa.

Kasoro hiyo inayohusu elimu ya msichana kuwa chini, wilayani Kisarawe iko wazi zaidi, hasa katika historia ya miaka ya nyuma, ikilinganishwa na sasa.

Kuna jitihada zilizofanyika, kupitia serikali, mashirika, taasisi na wadau wa elimu wengine wilayani.

**PLAN INTERNATIONAL**

Hapo ndipo inajitokeza nafasi ya asasi isiyo ya kiserikali ya Plan International, ambayo imekuwa ikitekeleza miradi yake mbalimbali kama elimu, afya, uwezeshaji vijana katika elimu na mitaji ya kiuchumi.

Wilayani Kisarawe, kuna elimu inayotolewa katika ngazi za shule za awali, msingi na sekondari. Jumla ya shule 21 za sekondari, sita kati yake ni binafsi na tano za serikali.

Ufaulu kwa watoto wa kike wilayani humo, ni tofauti ikilinganishwa na mtoto wa kiume. Wasichana wanafanya vibaya. Baadhi za sababu zinaelezwa ni kutokuwapo na miundombinu ya kielimu, kama mabweni kwenye shule za sekondari.

Ni hali inayotajwa kusababisha mwanafunzi kupata adha ya kutembea mbali kwenda shuleni na inaagukia katika sababu mojawapo ya wasichana kuangukia katika ujauzito ndani ya umri mdogo.

Ni maelezo yanayoishia katika simulizi ya msichana kuacha au kukatisha masomo yake na kutokumaliza elimu yake, pia, kuna hoja ya mabinti hao kuozeshwa katika umri mdogo.

Kampeni Tokomeza

Kutokana na sababu hizo, wilaya hiyo ilianzisha kampeni ya kupiga vita mimba, inayoitwa



Kutoka kulia, kiongozi wa Plan international Tanzania, Gweyneth Wong, Mkurugenzi Mtendaji wa wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe Mussa Gama, Mkurugenzi wa Plan International Ukanda wa Kusini Charles Businge na ofise wake, Marcely Madubi.

Tokomeza, mdau wake bega kwa bega ni shirika la Plan International. Hapo mtazamo mkuu ni kumjengea mazingira mwanafunzi afaulu na kuondoa ufuaulu duni kiwango cha 'ziro wilayani humo.

Wilaya hiyo ilianzisha kampeni mwaka 2017 katika ngazi zote za shule; elimu ya sekondari na msingi. Mabweni yalianza kujengwa shuleni, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

Inaelezwa, mara moja walipata ahadi na jumla ya vitu 945, ili kusaidia kuwapo kwa kiwango kikubwa mazingira yasiyo na na vishawishi, wakiwa nje ya masomo na makazi yao.

Mkurugenzi wa Plan International Kanda ya kusini, Charles Businge, aliyeambatana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisaware, Mussa Gama, anasema kampeni ya 'Tokomeza Ziro' imeonyesha mafanikio.

Gama anasema matunda yameshaonekana kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka juzi 'ziro' zimepungua kutoka 457 mwaka 2016 hadi 259.

Anasema, kwa kushirkiana na Plan International, ufaulu wa wanafunzi umeongezeka kwa asilimia 53 kutoka mwaka 2016 hadi asilimia 70.43 mwaka 2017.

"Kwa mfano, mwaka 2016 kulikuwa na kesi za mimba idadi iliongezeka na kufikia 27 mnamo mwaka 2017" anasema Gama.

**MBINU ZA KUHAMASISHA**

Gama anataja baadhi ya changamoto za elimu wilayani, ni wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shule, mimba za utotoni, kuacha shule, mila na desturi potofu. Anaeleza utatuzi wake ni kujenga shule mpya za sekondari za wasichana, inayoweza kutatua changamoto na kuinua uwezo wa msichana na maisha yake kwa ujumla.

Gama anafafanua kwamba katika mwaka uliopo, wilaya kwa kushirikiana na Plan International, wamejipanga kuboresha mazingira ya kufundishia, kuwahamasisha wasichana kwa kutumia watu maarufu na waliofanikiwa.

Anawataja mfano wa baadhi yao ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo, Makamu wa Rais Samia Suluhu na wadau wengine wanawake, wakiwamo wajumbe wa Bodi ya Wahandisi Wanawake na Bodi ya Wasanifu Majengo Wanawake.

Gama anasema ni namna ya kumhamasisha msichana akikua aone kuwa elimu ndio itamfanikisha kama wanawake wengine waliofanikiwa.

"Pia, tuna mpango wa kujenga miundombinu rafiki na hivyo kupunguza kutembea wa muda mrefu kwa wanafunzi hawa wa kike, hivyo kuongeza ufaulu, kupunguza mimba na kuacha shule" anasema

Gama anatoa mfano wa choo bora na cha kisasa katika Shule ya Palaka, iliyoko katika Kata ya Mkumbo, itakuwa msaada mkubwa kwa watoto wasichana kuyapenda mazingira ya shule.

Anaongeza kuwa shule hiyo mpya ya wasichana Kisarawe, itachangia kuongeza ufaulu wao na kutanua , idadi ya wasichana wanaoendelea na masomo ya juu, huku ikipunguza idadi ya wanaoacha shule na mimba.

Shule hiyo inakadiriwa kutumia fedha kati ya Sh. 1,514 na Sh. milioni mbili.

**SHULE YA MFANO**

Mkurugenzi wa shirika la Plan International Kanda ya Kusini, Charles Businge, anasema wameona umuhimu wa kumuwezesha msichana kwa kumsaidia kielimu na moja ya jitihada zao, ni kuwajengea miundombinu rafiki ya mabinti kupenda masomo.

Businge anasema, Plan International, imejenga madarasa katika shule mbalimbali wilayani, imetoa mafunzo kwa walimu, vifaa vya kufundishia kama vitabu, madaftari, madawati, kujenga vyoo na kumairisha usafi wa binti .

Businge anatumia mfano wa Shule ya Msingi ya Palaka, kwamba imejenga vyoo vya kisasa tisa na choo kimoja kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu.

Anasema ni maamuzi yanayotokana na ukweli kwamba, shule hiyo ina mazingira magumu na hayawezi kumuwezesha msichana kufikia malengo yake kielimu.

Businge anaielezea shule hiyo ni ya siku nyingi na vyoo vyake vimechakaa, hivyo kuwafanya baadhi ya wanafunzi wasipenda kwenda shule, wanajisaidia vichakani au jirani na shule, jambo ambalo ni hatari nyingine kwa msichana, dhidi ya vishawishi.

Mwalimu Mkuu shuleni hapo, Innocent Emmanuel, anaishukuru Plan international kwa msaada wa vyoo hivyo, kwani ni kitendo cha kuwaokoa wasichana shuleni, pia hatari ya magonjwa ya vichocho na mengineyo.



Mwanafunzi wa Klabu ya Afya Shule ya Palaka, akionyesha jinsi ya kutengeneza pedi za vitambaa. **PICHA ZOTE: ZUWENA SHAME:**



Anasema shule hiyo ilianzishwa mwaka 1968, ambayo ni miaka 51 iliyopita, ikiwa na matundu manne ya vyoo na wanafunzi 45, waliotumia madarasa mawili.

Hivi sasa shule hiyo ina madarasa saba, nyumba za walimu tatu, nyumba ya Mwalimu Mkuu na ofisi mbili za walimu. Mwalimu Emmanuel anasema, changamoto iliyokuwepo shuleni ni uchakavu wa madarasa, vyoo kwa ajili ya wavulana, changamoto ambayo Plan International kwa kushirikiana na wazazi, wameweza kuchangisha kufyatua matofali ya kujenga vyoo vya kisasa vya wavulana.

**WALIVYOSHINDA CHANGAMOTO**

Mwalimu Mkuu anasema, changamto kubwa shuleni kwake ni huduma ya wasichana kujisaidia, hasa wakati wakiwa kwenye hedhi na walijikuta hawahudhurii masomo shuleni.

Emannuel anaongeza kuwa, katika hiyo asasi ya Plan International, imewawezesha wasichana kwa kuwafundisha jinsi ya kutengeneza taulo za hedhi za asili, inayowapa ujasiri wa kuhudhuria masomo katika kipindi hicho kigumu.

"Kwa kweli tunashukuru shirika la Plan, kwani kwa sasa mtoto wa kike akiwa kwenye siku zake anahudhuria masomo kama kawaida.

# WAONDOA WASICHANA IA ZA MIMBA SHULENI



Mwanafunzi akipata huduma ya maji, kupitia mfumo rahisi uliobuniwa na Plan ernational katika Shule ya Msingi Palaka, Kisarawe.



Choo cha zamani (juu), na kipya katika sura tofauti, katika Shule ya Msingi Palaka Kisarawe. Huduma hiyo ilikuwa kikwazo katika shule hiyo kwa miaka 54.






Hakuna tena utoro, pedi hizi za kufua zinawasaidia sana," anasema Mwalimu Emmanuel.

Mwalimu wa Afya shuleni hapo, Husna Mohamed anayeshikilia jukumu hilo, anakiri Plan International, imewasaidia mafunzo hayo ya kutengeneza pedi za vitambaa, zinazowasaidia kuondokana na utoro wanapokuwa kwenye hedhi

Anasema, mwanzo wanafunzi walikuwa wanavaa vitambaa vya kawaida, vilivyowafanya wasiwe huru na kujiamini mbele ya wenzao.

Anasema, wadau hao waliwasaida mafunzo, pia kwa kwa ushirikiano na wazazi, wanafunzi wameshona pedi wakizitengeneza jumla pedi saba, inayompa uhuru wa kubadilisha hata katika siku tano za hedhi.

"Wanafunzi wa kike wamepokea kwa furaha sana ujio wa pedi hizi, zimewajengea watoto wetu uaminifu shuleni," anasema Mwalimu Husna.

**UGUMU ULIKO**

Anasema changamoto ya kikazi ni kwamba yuko peke yake shuleni hapo kwenye klabu ya afya, hivyo inakuwa vigumu kwa wanafunzi kuhudumiwa, iwapo anakuwa hayupo na mtoto kapata changamoto shuleni.


Pia, anaongeza kuwa kuna wanafunzi wengine wana uelewa duni, hivyo wanahitaji kufundishwa kwa umakini, jambo ambalo ni vigumu, katika upekee aliyo nao.

"Ningeomba tuongezewe mwalimu mwingine wa afya angalau tuwe wawili au watatu, kwani wanafunzi ni wengi na niko peke yangu" anashauri Mwalimu Husna.

Anasema, pia shuleni hapo wanafunzi hufundishwa njia salama na kisasa za kusafisha mikono, baada ya kutoka chooni, ili kujikinga na magonjwa ambukizi kama vile kip-

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 1 00)

Majibu toleo lijalo



**Kwenda kulia:**

1 Muda, majira
3 Mnyama wa kufugwa alaye Panya
5 Tabu
8 Hudumia mgonjwa
11 Chakula toka mbinguni walicholishwa Waisraeli
13 Maoni
14 Wingi wa neno Muungwana
17 Mtu dhaifu sana
18 Mtoto mchanga
19 Mwezi wa tano
20 Tafsiri ya jambo au kitu
22 Mkamilishaji wa mambo

**Kwenda Chini:**

1 Mashaka
2 Mtu anayeshikilia cheo fulani kwa muda
4 Funga imara, shika sana
6 Kiazi kikuu cheupe
7 Luanda ni mji wake mkuu
9 Hali ya kuwa raia
10 Fedheheka
12 Tokwa jasho
16 Sampuli ya simu
18 Chombo cha bati cha kuwekea vitu vidogovidogo
21 Dhamira

# Fahamu tabia za watoto wanaoishi gerezani na mama zao Kenya



Wadau nchini Kenya, wanataka sheria ibadilishwe ili mama anapohukumiwa na mtoto mchanga alee kwanza mtoto wake akiwa nje hadi pale atakapofikisha miaka minne, ndipo aendelee kutumikia kifungo chake. **PICHA: MTANDAO**

**NAIROBI, KENYA**

KWA miaka mingi sasa, wafungwa katika magereza ya wanawake nchini Kenya, wamekuwa wakiruhusiwa kukaa ndani na watoto wao hadi pale wanapotimiza miaka minne, ndipo watoto hao huachana na mama zao.

Lakini baadhi ya wanaharakati wa kupigania haki za binadamu wanasema si vizuri mtoto kuishi jela na mama yake kwani ananyimwa haki yake ya maisha bora. Wanataka sheria hiyo ibadilishwe.

BBC imezungumza na baadhi ya wahusika na kuandaa ripoti hii maalum ambayo pia inaangaza kwa undani maisha ya watoto hao gerezani, changamoto za mama wafungwa na watoto wao huko ndani na jinsi maisha hayo ya jela yanavyoathiri watoto hao kitabia.

Bernard Mbugua hatasahau maisha duni aliyoyapitia katika jela ya wanawake ya Lang'ata jijini Nairobi, akiwa mtoto wa chini ya umri wa miaka minne.

"Yalikua ni maisha ya shida, kuoga ni mara moja kwa wiki na mavazi pia ni tabu kwa watoto wengi hapo ndani," anasema Mbugua ambaye sasa ana umri wa miaka 18.

Mbugua hakuwa mfungwa katika jela hiyo ya Langata. Alijikuta yuko gerezani kwa makosa ya mama yake mzazi ambaye alihukumiwa kifungo cha miaka minne, baada ya kupatikana na kosa la kuuza pombe haramu.

Sheria ya Kenya kwa hivi sasa inamruhusu mama afungwe na mtoto wake wa chini ya umri wa miaka minne.

Hivyo, Mbugua akajikuta ni miongoni mwa watoto walioko gerezani lakini si wafungwa.

"Hayo maisha yetu tukiwa huko ni kama wafungwa tu kwa sababu hatuwezi kulala nje. Tena la kuudhi kabisa tunalala chumba kimoja, kitanda kimoja na mama zetu na wafungwa wengine ambao lugha yao chafu, si mfano mzuri kwa watoto wadogo wasio na hatia lakini wanajifunza matusi ya kila aina wanayosikia kwa wafungwa hao," anasema na kuongeza:

"Mimi sikubaliani kabisa na sheria hiyo ya watoto kufungwa na mama zao, iondolewe kwa sababu inamtesa mtoto... kama huna mtu anayekujua utajikuta umevaa mavazi hayo hayo mpaka yaanze kunuka baadaye."

Mashirika ya haki za kibinadamu yanapinga vikali sheria hii na wanataka ifutwe.

Wakfu wa Legal Resources Foundation Trust ni miongoni mwa wanaotaka sheria hiyo ya kuruhusu mama afungwe akiwa na mtoto wake ifutiliwe mbali.

Mratibu wa wakfu huo, Lenson Njagi Njogu anasema:

"Tunapinga vikali kuwekwa kwa watoto gerezani, kwani haki yake haijazingatiwa...watafute njia mbadala. Tushaanza kampeni ili sheria hiyo ipigwe marufuku na wahusika katika serikali ya Kenya."

Njogu anasema kwa hakika si sheria nzuri maanake inamnyima mtoto haki yake ya kukuzwa katika mazingira yafaayo, malezi bora, kwenda shule nzuri na kucheza na wenzake maeneo mazuri.

"Kwa mfano kule Afrika Kusini mama anapopatikana na hatia ya kufungwa jela na ana mtoto, kwanza anapewa nafasi ya kulea mtoto wake, kisha akifikisha zaidi ya umri wa miaka mitano anaingia jela sasa kutumikia kifungo chake," anasema.

Swali ni je, nchini Kenya inawezekana mama kupewa nafasi ya kumlea mwanaye na hatimaye kwenda jela kutumikia kifungo chake?

Baadhi ya raia wa nchi hiyo wanasema ni vigumu kwani mfungwa atajaribu kutoroka ahamie taifa lingine ama kaunti nyingine ili kuepuka kifungo hicho.

MAISHA GEREZANI

Maisha ya gerezani kwa mama wafungwa na watoto wao ni mzigo mkubwa, kama wanavyoeleza wafungwa waliozungumza na BBC katika jela ya wanawake ya Lang'ata mjini Nairobi.

"Mimi ni mama Saviour, nilikuja hapa Lang'ata mwaka wa 2017, Julai...maisha ya hapa si mazuri ni shida tupu... Pesa za matumizi kwa watoto wetu hatuna, hasa za kununua 'pampasi'. Nguo pia ni shida mpaka wageni waje watusaidie. Hapa tunatesa mtoto kwa sababu hana hatia, ni uchungu sana kufungwa na mtoto wako," anasema.

**MAMA KAMAU**

Kwa upande wake Mama Kamau ama Jacqueline kwa jina lake naye anapendekeza wapate kifungo cha nje na watoto wao, kuepuka maisha magumu ya jela.

"Mtoto hana makosa hata kidogo, sioni kwa nini niwe naye hapa. Lakini pia ni shida akibaki nje kwa sababu hakuna mtu wa kumuangalia...nasikia vibaya sana kuwa na mtoto wangu hapa ndani... Maisha yake yote anajua tu askari jela na polisi," anasema.

Kwa hivi sasa jela ya wanawake ya Lang'ata ina jumla ya watoto 32, na ni jukumu la jela hiyo kuwalea watoto hao na mama zao.

Mkuu wa jela hiyo ya wanawake Jane Kiiri, anasema miongoni mwa changamoto zinazowakabili wafungwa hao, zinachangia watoto wao kutopata malezi bora.

"Hawa kina mama wanapokuwa hapa jela wana mawazo mengi sana. Wanafikiria watoto wao waliowaacha nje wanakula nini, kwa hivyo inakuwa vugumu hata kuwapa watoto wao wachanga malezi bora," anasema na kuongeza:

"Mavazi ni shida kwa sababu hatuna bajeti yake, sasa ndio tutajaribu kuzungumza na serikali watusaidie. Vyakula pia ni shida na wanapougua kuwapa matibabu ni mzigo mkubwa kwetu hapa gerezani."

Jane anaomba wadhamini wanaojiweza wasaidie kwa hali na mali kwa sababu mzigo huo wanaoubeba ni mzito mno.

" Wanasaikolojia pia tunahitaji huduma zao... waje kuzungumza na mama hawa wafungwa," anasema.

Maisha hayo ya gerezani yana athari zake, kama asemavyo Jane Onyango ambaye ni ofisa mkuu wa kuangalia maslahi ya wafungwa jela ya Lang'ata.

"Watoto hawa kufungwa na mama ina athari zake wakiwa wakubwa," anasema Onyango na kuongeza:

"Huyo mtoto hataogopa kufanya kosa huko nje afungwe kwa sababu alipokuwa jela hakuna kazi alifanya ama kuadhibiwa. Kwa hivyo kwake anaona maisha jela ni ya starehe, kula na kulala."

Onyango anasema watoto hao wanapotimiza miaka minne kisheria huachiwa waende kwenye vituo vya kusimamia watoto kwa sababu wakiwa huko jela katika umri huo, ni wa kuelewa kabisa mambo yanayoendelea jela.

"Siku ya watoto hao kuondoka huwa ni ya majonzi kwa mama wafungwa kuachana na watoto wao, lakini inabidi," anasema Onyango na kuongeza:

"Hata hivyo, wakiwa katika vituo vya kulea watoto sisi hupanga siku maalum ambapo watoto huletwa kujiunga na wazazi wao, wale vizuri na wanywe pamoja kisha wanarudishwa huko...hii ni kuhakikisha hatumnyimi mtoto haki ya kumtembelea mama yake."

Wengi wa watoto hao hupelekwa kituo cha kulea watoto kiitwacho Nest Childrens Home eneo la Limuru.

Ni kama umbali wa kilomita 40 kutoka katikati ya jiji la Nairobi.

**LUCY NDUTA**

Lucy Nduta ni mmoja wa wahudumu wa kituo hicho cha Nest Childrens Home kilichoanzishwa miaka 27 iliyopita na mkurugenzi mkuu, Irene Baumgartner kutoka Ujerumani.

"Hapa tunalea zaidi ya watoto 70 wa wafungwa katika jela za wanawake sehemu mbalimbali za Kenya," anasema Nduta.

"Tuko pia na watoto ambao wamekosa malezi bora huko nje ama wameachwa na wazazi wao... hawa mama wafungwa wanapoachiwa wanakuja hapa, tunawapa malazi na watoto wao ili waanze kuzoeana baada ya kutengana kwa muda mrefu. Tunawaelimisha, kuwavalisha na kuwasomesha. Huu ni mzigo ambao tunaomba wahisani watusaidie."

Anaongeza:

Nduta anaeleza jinsi wanavyokuwa na shida kubwa ya kulea watoto ambao hufungwa na mama zao katika jela za wanawake nchini Kenya.

"Unajua hawa watoto wametoka mahali walikokuwa wanaishi maisha magumu. Sasa tabia zao na lugha ni tofauti kabisa na hawa watoto wengine ambao hawakuwa jela."

Anabainisha kuwa lugha yao huwa ni ya matusi na wanapenda vita.

"Wakiwa kwenye mabweni utawajua kwa tabia zao chafu, maanake hayo mambo wameyaona yote huko jela... ukiwapa vitu vya watoto vya kuchezea hawataki mwenzao karibu. Ni wagumu sana kulea na hii inatokana na wao kuishi jela,"anasema.

Na ndio maana wakfu wa Legal Resources Foundation Trust wanapinga kabisa mtoto kuwa gerezani na mama yake.

Kwa mujibu wa mratibu wa wakfu huo, wanakaribia kufaulu kuishawishi serikali iondoe sheria hiyo inayomruhusu mama afungwe jela na mtoto wake aliye chini ya umri wa miaka minne.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA KILIMO

**MHUTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2019/2020**



*Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga (Mb)*
Waziri wa KILIMO



*Mhe. Omary Tebweta Mgumba (Mb)*
Naibu Waziri KILIMO



*Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb)*
Naibu Waziri KILIMO



*Eng. Mathew John Mtigumwe –*
Katibu Mkuu KILIMO



*Prof. Siza Donald Tumbo –*
Naibu Katibu Mkuu KILIMO

# MHUTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2019/2020

**MEI, 2019**

**1.0 UTANGULIZI**

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

***2.*** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima wa afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani na mshikamano na kujadili bajeti hii inayolenga kusukuma mbele kasi ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo na wakulima kwa ujumla wao.

***3.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Pia, niwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayofanya kusukuma maendeleo ya nchi hii, ikiwemo Sekta ya Kilimo. Napenda kuwaahidi kwamba nitafanya kazi ya kuongoza Wizara ya Kilimo kwa uaminifu, juhudi na maarifa ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo zinawafikia walengwa ili kuongeza tija na kuinua kipato chao.

***4.*** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake ambayo iligusa maeneo mengi ikiwemo Sekta ya Kilimo. Aidha, nimpongeze tena Mhe. Waziri Mkuu kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele kuhamasisha na kusimamia kilimo pamoja na maendeleo ya Vyama vya Ushirika.

***5.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa.
Aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote kwa umahiri wao mkubwa katika mijadala inayoendelea katika Bunge hili la Bajeti.

***6.*** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji chini ya Uenyekiti wa Mhe. Mahmoud Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu Mwenyekiti Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma (Mb). Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wizara na kutembelea baadhi ya maeneo kuona utekelezaji wa kazi za kilimo na kushauri namna ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Bodi na Taasisi zake. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, ushauri wao umezingatiwa na tutaendelea kushirikiana na Kamati ili kuleta mageuzi ya kilimo nchini.

**2.0 MWELEKEO WA SEKTA YA KILIMO**

***7.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imepanga kubadilisha kilimo kutoka kuwa cha kujikimu na kuwa kilimo cha kibiashara kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo umesisitizia mapinduzi ya viwanda na umeitambua Sekta ya Kilimo kuwa mhimili imara kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwanda. Miongozo hiyo ya Kitaifa, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Sera ya Kilimo ya mwaka 2013, inatekelezwa na Wizara kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ambayo inalenga kuleta mageuzi katika Sekta ya Kilimo. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza mitaji, teknolojia na ubunifu, Sekta Binafsi inashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa ASDP II.

***8.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ASDP II iliyozinduliwa rasmi tarehe 4 Juni, 2018 na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inalenga kubadilisha maisha ya mkulima kwa kufanya mageuzi makubwa kwenye kilimo kwa kuzingatia mazao ya kipaumbele kulingana na ikolojia za kilimo.

**3.0 MCHANGO WA KILIMO KATIKA UCHUMI**

***9.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kilimo ni sekta kubwa na muhimu kwa maendeleo kutokana na mchango wake katika uchumi. Katika mwaka 2017, sekta hiyo imetoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 65.5, ikichangia takriban asilimia 28.7 ya Pato la Taifa ambapo sekta ndogo ya mazao ilichangia asilimia 16.58. Vilevile, Sekta ya Kilimo inachangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda. Takwimu zinaonesha kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2018, ukuaji wa Sekta ya Kilimo ulifikia asilimia 7.1. Ukuaji huo ulichangiwa na jitihada za Serikali za kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya pembejeo bora, hali nzuri ya mvua na uboreshaji wa miundombinu ya uzalishaji.

**3.1 Upatikanaji wa Chakula**

***10.*** ***Mheshimiwa Spika,*** upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 ulifikia tani milioni 16.89 zikiwemo tani milioni 9.53 za mazao ya nafaka na tani milioni 7.35 za mazao yasiyo nafaka. Kiwango hicho cha uzalishaji kimeiwezesha nchi kujitosheleza kwa mahitaji yake ya chakula ya tani milioni 13.56 na hivyo kuwa na ziada ya tani milioni 3.32 za chakula kwa kiwango cha utoshelevu cha asilimia 124. Niwahakikishie watanzania kwamba, tunacho chakula cha kutosha nchini. Hata hivyo, tuendelee kuweka akiba katika kaya zetu hadi tutakapovuna tena kwani inaonekana kwamba huenda tusiwe na mavuno mazuri sana msimu huu kutokana na uhaba wa mvua kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa, Kati na Kaskazini mwa nchi yetu. ***(Maelezo ya kina yanapatikana uk.5 wa kitabu cha Hotuba ya bajeti).***

**3.2 Umwagiliaji**

***11.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ili kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kuzingatia Mipango Shirikishi ya Maendeleo ya Rasilimali za Maji. Katika mpango huo, hekta 560,880 zimepangwa kuendelezwa kwa lengo la kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 475,052 mwaka 2018/2019 hadi hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2035. ***(Maelezo ya kina yanapatikana uk.6 wa kitabu cha Hotuba ya bajeti)***

**3.3 Maendeleo ya Ushirika**

***12.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kuimarisha Sekta ya Ushirika kwa kusimamia na kuhamasisha maendeleo yake. Vyama vya Ushirika vimeongezeka kutoka vyama 10,990 Desemba 2017 hadi vyama 11,331 kufikia Desemba 2018. Vilevile, idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika imeongezeka kutoka 2,619,311 mwaka 2017 hadi 3,998,193 Februari, 2019 sawa na ongezeko la asilimia 53. Hadi Desemba 2018, mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.3 imetolewa kwa wanachama ikilinganishwa na Shilingi bilioni 902 iliyotolewa kufikia Desemba 2017.

Aidha, Akiba na Amana za wanachama katika SACCOS zimefikia Shilingi bilioni 575 na hisa Shilingi bilioni 79. ***(Maelezo ya kina yanapatikana uk.7 wa kitabu cha Hotuba ya bajeti)***

**4.0 UTEKELEZAJI WA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2018/2019**

**13. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara imetekeleza maeneo ya kipaumbele ya kuongeza tija kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, udhibiti wa visumbufu, matumizi ya zana bora za kilimo na huduma za ugani; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo na masoko; kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha teknolojia kwa mazao ya mahindi, muhogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba na mpunga.

14. Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya kipaumbele ni kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za mazao na kusambaza kwa wakulima; kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti; kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo ki-ikolojia; mafunzo na usambazaji taarifa za kilimo na sayansi shirikishi; kusajili na kuandaa kanzidata ya wakulima na kuimarisha ushirika. ***(masuala yote ya utekelezaji wa maeneo ya kipaubele yapo kwa kina kwenye ukurasa 10-61 katika kitabu cha Hotuba ya bajeti)***

***15.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele hivyo, Shilingi bilion**i 204.07** ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo, Fungu 43 – Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa Shilingi bilioni **166.26** zikiwemo Shilingi bilioni **68.14** za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni **98.12** za matumizi ya maendeleo; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 05 iliidhinishiwa Shilingi bilioni **29.77** zikiwemo Shilingi bilioni **3.95** za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni **25.82** fedha za maendeleo; na Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 iliidhinishiwa Shilingi bilioni **8.05** zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida.

**4.1 Kuongeza Tija katika Kilimo**

**Upatikanaji wa mbegu bora za mazao**

***16.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 49,040.66. Kati ya kiasi hicho, tani 38,507.87 zimezalishwa hapa nchini, tani 8,361.46 zimeagizwa toka nje ya nchi na tani 2,171.33 ni bakaa ya msimu wa 2017/2018. Vilevile, miche 1,507 ya miwa, vipando 121,805 vya muhogo na vikonyo 520,000 vya viazi lishe vimezalishwa. Aidha, aina mpya 13 za mbegu bora zimeidhinishwa na zitaanza kuzalishwa msimu wa 2019/2020.

**Upatikanaji na udhibiti wa ubora wa Mbolea**

***17.*** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2019, upatikanaji na usambazaji wa mbolea nchini ulikuwa tani 492,394 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 514,138 katika msimu wa 2018/2019. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imefanya ukaguzi kwa wauzaji wa mbolea 1,350 na wafanyabiashara 496 wapya wa mbolea wamesajiliwa.

**Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu**

***18.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imenunua lita 296,000 na kilo 3,000 za viuatilifu vyenye thamani ya Shilingi bilioni tisa (9) kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao. Hadi kufikia Machi 2019, ndege waharibifu wa nafaka walidhibitiwa katika skimu za umwagiliaji za Kahe, Lekitatu na Misenyi kwa mazao ya mpunga na mtama. Aidha, lita 119,000 kwa ajili ya kudhibiti Viwavijeshi Vamizi zimesambazwa katika Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki na kutoa mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima 350.

**Zana za Kilimo**

19. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba wastani wa kitaifa wa matumizi ya zana bora za kilimo umeongezeka hadi kufikia asilimia 20 kwa matrekta na asilimia 27 kwa wanyama kazi ikilinganishwa na asilimia 14 ya matrekta na asilimia 24 ya wanyama kazi mwaka 2013. Kutokana na ongezeko hilo, matumizi ya jembe la mkono yamepungua na kufikia asilimia 53 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 62 kwa mwaka 2013. Aidha, kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) Wizara imendelea kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, mikopo 33 yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.50 imetolewa.

**4.2 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

***20.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Umwagiliaji imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo unaofadhiliwa na Serikali ya Japan. Mradi

# HOTUBA WIZARA YA KILIMO

umekarabati skimu za umwagiliaji 129 katika Halmashauri 68 nchini pamoja na ununuzi wa mitambo ya ujenzi.

**4.3 Utafiti wa Kilimo na Uhaulishaji wa Teknolojia**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TARI imegundua mbegu bora mpya aina nne (4) za mahindi. Mbegu hizo zina uwezo wa kutoa mavuno kwa wastani wa tani 5.8 kwa hekta kwenye mashamba ya wakulima katika ukanda wa chini na kati, zinahimili ukame na zina ukinzani wa magonjwa ya majani ya mahindi na michirizi na ukungu. Vilevile, kwa kushirikiana na kampuni binafsi, TARI imezalisha aina sita (6) ya miche ya mbegu bora ya migomba na kugundua aina 62 za mbegu za mazao ya mikunde.

**4.4 Maendeleo ya Mazao**

22. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao mbalimbali kwa kuimarisha huduma za utafiti, upatikanaji na utumiaji wa pembejeo na zana za kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mazao, huduma za ugani, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko. Aidha, Wizara imeandaa mkakati wa miaka minne (2018/2019 – 2021/2022) wa kuendeleza zao la michikichi.

**Mazao Makuu ya Asili ya Biashara**

23. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara uliongezeka kutoka tani 901,641 msimu wa 2016/2017 hadi tani 967,184 msimu wa 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.2. Katika msimu wa 2018/2019, Wizara ililenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara hadi kufikia tani 1,356,368 na hadi kufikia Machi 2019, tani 667,631.77 sawa na asilimia 49.2 ya lengo zilikuwa zimezalishwa na uzalishaji unaendelea.

**Mazao ya Bustani**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, uzalishaji wa mazao ya bustani ulikuwa tani milioni 5.33 na matarajio ya uzalishaji kwa mwaka 2018/2019 ni tani milioni 5.96. Hadi Machi 2019, uzalishaji umefikia tani milioni 4.36 sawa na asilimia 73.17 ya lengo na msimu wa uzalishaji unaendelea.

**4.5 Ujenzi wa Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo na Masoko**

**Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo**

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) inaendelea kutekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, asilimia 83 ya vifaa vilikuwa vimeingizwa nchini kwa ajili ya ujenzi wa ghala katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma.

**Masoko ya Mazao ya Kilimo**

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeanzisha kitengo cha masoko ya mazao ya kilimo ambacho kinahusika na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeingia makubaliano ya Itifaki ya Usafi baina ya Tanzania na Serikali ya China kuwezesha kuuza muhogo nchini China ambapo hadi mwezi Machi 2019, kampuni tano zimesajiliwa kwa ajili ya kuuza zao hilo nchini China.

**Hifadhi na Usalama wa Chakula**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, NFRA imenunua tani 46,236.035 za mahindi kwa ajili hifadhi na imeliuzia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani tani 36,000 za mahindi zenye thamani ya Shilingi bilioni 21. Aidha, Wizara imeanza kutekeleza Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu katika mazao unaolenga kudhibiti tatizo la sumukuvu katika mazao ya mahindi na karanga.

**4.6 Huduma za Ushauri Kuhusu Utafiti, Mafunzo na Usambazaji Taarifa za Kilimo na Sayansi Shirikishi**

**Huduma za Ugani**

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Utoaji na usimamizi wa huduma za ugani utakaotumiwa na Sekta ya Umma na Binafsi. Aidha, elimu kuhusu kanuni bora za uzalishaji wa mazao, kuongeza thamani mazao ya kilimo, upatikanaji wa masoko, mitaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo, pembejeo na zana bora za kilimo imetolewa kupitia maonesho na vyombo vya habari.

**Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Vyuo vyake vya Kilimo imedahili na kufundisha wanafunzi 2,389 ambapo wanafunzi 2,051 wamefadhiliwa na Serikali na 338 wanajilipia wenyewe. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, wanafunzi 1,537 ni ngazi ya Astashahada na 852 ni ngazi ya Stashahada. Jumla ya wanafunzi 1,026 wakiwemo 263 wa Stashahada na 763 wa Astashahada watahitimu masomo yao mwezi Juni, 2019.

**4.7 Kuimarisha Ushirika**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Tume ya Maendeleo ya Ushirika kupitia Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) limefanya ukaguzi wa nje kwa vyama vya ushirika 2,297. Kati ya Vyama vilivyokaguliwa, asilimia 4.6 vilipata hati inayoridhisha, asilimia 64.6 vilipata hati yenye shaka, asilimia 21.6 vilipata hati isiyoridhisha na asilimia 9.2 vilipata hati mbaya. Hali hiyo ya Vyama vya Ushirika siyo nzuri na hatuwezi kuifumbia macho. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yetu tuendelee kushirikiana na Halmashauri zetu kuvisaidia vyama hivi ambavyo ni mkombozi wa mkulima.

**4.8 Usajili wa Wakulima**

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanza usajili wakulima wote kwa mazao ambayo yanasimamiwa na Bodi. Mazao hayo ni, kahawa, korosho, miwa, pamba, chai, mkonge, tumbaku na pareto. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, wakulima 1,464,827 wametambuliwa na kusajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**4.9 Masuala Mtambuka**

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kuzingatia masuala mtambuka katika kutekeleza majukumu yake. Masuala hayo ni pamoja na ushiriki wa vijana katika kilimo, lishe, jinsia, hifadhi ya mazingira na VVU na UKIMWI.

**5.0 MPANGO NA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2019/2020**

**5.1 Kuongeza Tija katika Kilimo**

**Upatikanaji wa mbegu bora za mazao**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, imejipanga kuzalisha jumla ya tani 53,608.2 za mbegu mbalimbali. Wazalishaji hao ni pamoja na ASA, Vituo vya Utafiti, Magereza na Sekta binafsi. Vilevile, ASA itazalisha vipando bora vya mihogo pingili 7,000,000 na miche bora ya matunda 20,000. Ili kufikia malengo hayo, miundombinu ya umwagiliaji itaboreshwa katika mashamba yanayomilikiwa na ASA na eneo la uzalishaji wa mbegu litaongezwa hadi kufikia hekta 811 katika mashamba mbalimbali.

**Upatikanaji na udhibiti wa ubora wa Mbolea**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itasimamia uagizaji na usambazaji wa tani 625,000 za mbolea zinazokadiriwa kutumika nchini. Aidha, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) itaongeza mauzo ya mbolea kutoka tani 10,000 hadi tani 100,000. Vilevile, ghala moja (1) lenye uwezo wa kuhifadhi tani 20,000 za mbolea litakarabatiwa katika wilaya ya Tabora pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchanganya mbolea kwa uwiano (blending plant) katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itanunua na kusambaza lita 300,000 na kilo 3,000 za viuatilifu kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha kituo cha kudhibiti milipuko cha Kilimo Anga (Arusha) ili kutoa huduma bora. Vilevile, Wizara itaendelea kuvijengea uwezo na kukarabati vituo 10 kati ya 36 vya ukaguzi wa mazao mipakani.

**Zana za Kilimo**

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaanzisha kituo kimoja (1) cha zana za kilimo kwa ajili ya kutoa huduma za kiufundi na mafunzo kwa watoa huduma binafsi wamiliki na watumiaji wa zana za kilimo kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wakulima katika Kanda ya Ziwa. Vilevile, Wizara kupitia AGITF, imepanga kutoa mikopo 250 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.12.

**5.2 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itafanya tathmini ya miradi ya umwagiliaji ambayo ujenzi wake haujakamilika ili miradi hiyo iweze kukamilishwa kwa awamu.
Aidha, kupitia Mradi wa Kuendeleza Skimu za Wamwagiliaji Wadogo, Wizara itakamilisha ujenzi wa skimu 16 za umwagiliaji katika maeneo mbalimbali.

**5.3 Utafiti wa Kilimo na Uhaulishaji wa Teknolojia**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TARI imepanga kutafiti, kugundua na kusambaza aina 15 za mbegu bora za mazao ya nafaka, mizizi, mbegu za mafuta, mikunde, migomba na mazao ya bustani. Vilevile, Wizara itasafisha aina tisa (9) za mbegu za mpunga na kuzalisha tani 10 za mbegu za awali katika Kituo cha Utafiti cha KATRINI. Aidha, kupitia kituo cha TARI Naliendele, Serikali itajenga kinu cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 1,800 kwa mwaka na kusindika tani 1,000 za mvinyo na sharubati (juice).

**5.4 Maendeleo ya Mazao**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya kipaumbele kwa kuendelea kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao hayo ikiwemo kuimarisha utafiti, upatikanaji na utumiaji wa pembejeo na zana za kilimo, udhibiti wa visumbufu, huduma za ugani, kuongeza maeneo ya uzalishaji, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko.

**Zao la Korosho**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Korosho itaendelea kutekeleza programu ya kuzalisha miche bora milioni 10 ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.
Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itahakiki na kulipa vikundi vya wazalisha miche ya mikorosho kwa msimu wa 2017/2018 ambao hawajalipwa katika mikoa saba (7). Vilevile, Wizara itaratibu upatikanaji na usambazaji wa tani 30,000 na lita 500,000 za salfa kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la korosho.

**Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Sukari itaratibu uzalishaji wa tani 403,786 za sukari kwa kuongeza eneo la uzalishaji wa kilimo cha miwa kutoka hekta 52,000 hadi hekta 97,000. Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) itawezesha upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji wa miradi mipya ya sukari katika Wilaya za Kasulu, Kibondo, Rufiji, Geita, Kilombero, Karagwe, Pangani, Bagamoyo na Morogoro.

**Zao la Kahawa**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya kahawa itaongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 65,000 hadi tani 80,000. Aidha Bodi imepanga kuzalisha na kusambaza miche milioni 10 ya kahawa katika Wilaya 42.

Zao la Mkonge

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge imepanga kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 38,506 hadi tani 113,506 kwa kuongeza eneo la uzalishaji kutoka hekta 42,426.11 hadi 114,915.08, kusimamia uendeshaji wa mfumo wa kilimo cha wakulima wadogo cha mkataba na kuimarisha vyama vya ushirika na masoko ya mkonge.

**Zao la Pamba**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Pamba imepanga kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 222,000 hadi tani 700,000 na tija kutoka tani 300 hadi tani 600 kwa ekari. Aidha, upatikanaji wa mbegu za pamba utaongezeka kutoka tani 22,000 hadi 40,000 na upatikanaji wa viuatilifu utaongezeka kutoka lita milioni 7 hadi milioni 10.

**Zao la Tumbaku**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku imepanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 55,000 hadi tani 60,000; kuimarisha vituo 1,972 vya kufungia na kuchambulia tumbaku; itaimarisha mfumo wa

# HOTUBA WIZARA YA KILIMO

upatikanaji wa pembejeo za zao la tumbaku kwa kuwaunganisha watoa huduma wa pembejeo na Vyama vya Ushirika ili ziwafikie kwa wakati.

Zao la Chai

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Chai imepanga kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 34,000 hadi tani 40,000 ambazo ni sawa na tani 182,000 za majani mabichi ya chai. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) itafufua kiwanda cha chai cha Mponde ili kuimarisha upatikanaji wa soko la majani mabichi ya chai kwa wakulima na kuongeza ajira.

**5.5 Miundombinu ya Hifadhi na Uongezaji Thamani Mazao ya Kilimo**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia NFRA itakamilisha awamu ya kwanza ya Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi ambapo ujenzi wa maghala matano (5) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 na vihenge nane (8) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 za nafaka utakamilika na hivyo kuongeza uwezo wake wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 251,000 hadi tani 501,000.

**5.6 Vituo vya Utafiti huduma za Ugani na Mafunzo Kuimarisha Vituo vya Utafiti**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itakarabati ofisi na kuvipatia vifaa muhimu vituo vya utafiti vya Ukiliguru, Ilonga na Tumbi. Aidha, miundombinu ya umwagiliaji ya vituo vya utafiti vya Ilonga, Naliendele, Ukiliguru na miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Seliani itaboreshwa.

**Huduma za Ugani**

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Sekta binafsi itakamilisha Mwongozo wa Utoaji na Usimamizi wa Huduma za Ugani Kilimo ili kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za ugani nchini.

**Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itadahili wanafunzi 2,500 ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa ufadhili wa Serikali. Vilevile, itakarabati miundombinu ikiwa ni pamoja na madarasa sita (6), ofisi 12, mabweni 12, maktaba sita (6) na mabwalo ya chakula sita (6) katika vyuo vya mafunzo ya kilimo vya Mtwara, Igurusi, HORTI Tengeru, Tumbi, Mlingano na Maruku.

**5.7 Kuimarisha Ushirika**

51. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama vya ushirika; itahamasisha wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Mazao kuanzisha SACCOS 1,500 kwenye maeneo yao; na itahuisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 na kuipitia upya sheria za ushirika.

**5.8 Uratibu, Takwimu, Ufuatiliaji na Tathmini**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar itafanya Sensa ya kilimo.

**5.9 Masuala Mtambuka**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuzingatia masuala mtambuka yakiwemo ushiriki wa vijana katika kilimo, lishe, jinsia, VVU na UKIMWI na mazingira katika utekelezaji wa majukumu yake.

5.10 Maeneo Maalum ya Maboresho katika Kilimo

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nizungumzie maeneo machache ya kimkakati ambayo kama Wizara tumeona ni muhimu kuyafanyia maboresho ili kuimarisha usimamizi wa kilimo na kuwapatia wakulima huduma kwa urahisi zaidi. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

**Mapitio ya Sera na Sheria**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanza na itaendelea kuipitia Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 na sheria mbalimbali kwa lengo la kubaini maeneo ambayo yatapaswa kuhuishwa ili kwenda na hali halisi ya sasa na mwelekeo wa Serikali wa kubadili kilimo chetu kuwa kilimo cha kibiashara. Mtazamo wa Wizara ni kuwa na Sheria moja itakayosimamia rasilimaliwatu, matumizi bora ya pembejeo, ardhi ya kilimo na maeneo mengine muhimu.

**Bima ya Mazao**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza mchakato wa kuanzisha Bima ya Mazao hapa nchini ili kumwezesha mkulima kulipwa fidia pale anapopata hasara. Maandalizi yanaendelea kufanyika ili katika mwaka 2019/2020 tuwe angalau na aina mbili za mifumo ya Bima ya mazao inayoweza kutumika hapa nchini. Hata hivyo, ili utaratibu huu uwezekane, kutahitajika takwimu sahihi za hali ya hewa pamoja na uzingatiaji wa kanuni bora za Kilimo.

**Usajili wa wakulima**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaimarisha kanzidata ya wakulima na kuendelea na usajili wa wakulima wa mazao mchanganyiko kwa kushirikiana kwa karibu sana na Vyama vya Ushirika na Taasisi nyingine kilele za wakulima kama vile Tanganyika Farmers Association (TFA). Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuhamasisha wakulima katika maeneo yetu ili watakapofikiwa na zoezi la uandikishaji watoe ushirikiano na waelewe kwamba zoezi hili ni la kuwasaidia kupata huduma bora za Kilimo.

**Masoko ya Mazao ya Kilimo**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeamua kuimarisha utafutaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itakiimarisha kitengo cha masoko kwa kukijengea uwezo wa kufanya uchambuzi na utafutaji wa masoko ndani na nje ya nchi.

Aidha, elimu itaendelea kutolewa kwa wakulima ili wazalishe kulingana na mahitaji ya soko. Vilevile, tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na taasisi nyingine zinazohusika na masoko nchini ikiwemo TANTRADE na Soko la Bidhaa (TMX).

**Mfumo wa upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanza zoezi la kupitia kwa kina mifumo iliyopo ya uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa mbegu, mbolea na viuatilifu. Mifumo iliyopo kwa sasa inatofautiana kwani kuna baadhi ya Bodi za Mazao zinazojihusisha na uagizaji na usambazaji wa pembejeo, wakati mwingine Vyama vya Ushirika vinaagiza na kusambaza pembejeo kwa wanachama wao, wakulima pia hununua pembejeo moja kwa moja kutoka kwa wafanyabiashara na pia mbolea kwa sasa inaagizwa kwa mfumo wa pamoja (Bulk Procurement).

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na umuhimu wa pembejeo za kilimo na tofuati ya mifumo hiyo, tumeamua kuipitia yote ili kuona mfumo bora unaoweza kutumika kuhakikisha pembejeo zenye ubora zinapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati. Malengo yetu ni kukamilisha mapitio hayo na kupata majawabu ya mfumo bora ifikapo Juni 2019, ili mwaka 2019/2020 tuwe na mfumo madhubuti utakaokuwa na tija kwetu sote. Nina uhakika kwamba, mfumo mzuri wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo utawezesha uwepo wa pembejeo bora kwa bei nafuu na hivyo kuongeza matumizi kwa wakulima wetu.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina ya hotuba yangu hususan mpango na maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2019/2020 yanapatikana ukurasa wa 61 hadi 91 katika kitabu cha hotuba cha Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2019/2020 kilichowasilishwa Bungeni.

**6.0 SHUKRANI**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijamaliza hotuba yangu naomba nitoe shukrani za dhati kwa watu, taasisi, makundi na wadau mbalimbali ambao tunashirikiana kuendeleza kilimo. Kwanza, nawashukuru sana, Naibu Mawaziri wa Kilimo, Mhe. Omary Tebweta Mgumba (Mb.) na Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb.) kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Napenda pia, kuwashukuru Katibu Mkuu, Mhandisi Mathew John Mtigumwe; Naibu Katibu Mkuu, Prof. Siza D. Tumbo; Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na wadau wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 pamoja na kuandaa Hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, nitaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2019/2020.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam, Canada na Poland. Ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI na CABI. Nyingine ni CFC, AVRDC, AGRA, CIP, CIAT/PABRA, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani na HELVETAS. Wadau wengine ni Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu, Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust, Rockfeller Foundation, Aga Khan Foundation, Unilever na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote hapa.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Vwawa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, napenda kuwahimiza kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu wa kipekee ninatoa shukrani za dhati, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

**7.0 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2019/2020**

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara inaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya Shilingi **3,472,515,000** yatokanayo na vyanzo mbalimbali vya mapato.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Kilimo inaomba kutumia jumla ya Shilingi **253,856,943,970** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kama ifuatavyo;

**FUNGU 43 – Wizara ya Kilimo**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **208,044,783,**140 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **143,577,036,140** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **82,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **61,577,036,140** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **64,467,747,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **13,214,159,060** ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara, Shilingi **29,621,801,490** ni kwa ajili ya mishahara ya Bodi na Taasisi, Shilingi **11,453,309,490** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara na Shilingi **10,178,476,510** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Bodi na Taasisi.

**FUNGU 05 – Tume ya Umwagiliaji**

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **37,485,090,830** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **32,501,462,613** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi **3,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **29,501,462,613** ni fedha za nje.

Aidha, Shilingi **4,983,628,217** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **4,098,444,217** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume na Shilingi **885,184,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**FUNGU 24 – TUME YA USHIRIKA**

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **8,327,070,000** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **6,127,370,000** kwa ajili ya mishahara na Shilingi **2,199,700,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Maelezo ya sehemu ya maombi ya fedha mwaka 2019/2020 kwa fungu 43, 65 na fungu 24 yanapatikana ukurasa wa 93 hadi 95 katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

**HITIMISHO**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na hotuba hii, vipo viambatisho vinavyotoa ufafanuzi wa baadhi ya maeneo. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Kilimo, www.kilimo.go.tz. Ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** **NAOMBA KUTOA HOJA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.

## MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA**,NYUMBA INAUZWA YENYE VYUMBA SITA, UZIO NA NAFASI KUBWA, MAJI YAPO, IPO TEMEKE JIRANI NA SHULE YA SANDALI, BARAZA LA KATA. BEI NI NAFUU. PIGA SIMU: 0719 698680, 0654 766168, 0762 014266. MADALALI HAWATAKIWI.

**MONKAL I INSULIN:** Inaponya maradhi mbalimbali sugu kwa waliogua muda mrefu,inarejesha kongosho ktk utoaji ute mchungu na kuwa normal balance 4- 5- 6, iko katika mfumo wa maji na vidonge,husaidia mmengenyo wa chakula,tiba lishe,gout,vidonda vya tumbo kuunguruma na kujaa gesi n.k kama umehangaika huku na kule bila mafanikio njoo nikusaidie acha kuteseka:0713293988/0758078288

NIPASHE NI JIBU LAKO

## CHETI KIMEPOTEA



**JOSEPH PETER MBASHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0110/0058** kilichotolewa na ILBORU SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TBT/RB/873/2013.**

115235302

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHRISTINA PETER LAIZER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba P.0327-0006** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari Minja Tech . Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chaochote cha Polisi. Polisi Taarifa:**MOR/RB/4471/2019**

115234702

## KUPOTEA KWA CHETI



**NNINGE N. NTALE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1363/0322** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Temboni . Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chaochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **SRB/RB/1308/2019**

115234602

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAVID MATHEW KILIKINI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.4202-0018** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Francis Maria Libermann. Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chaochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KYN/RB/224/2019**

115234802

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
17/05/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe **24/05/2019** kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MOROGORO kuelekea NAMANGA** gari hilo lenye namba za usajili: **T 188 APK, T741 CPB, T 329 BKM.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu -mita 17**
   **Upana –mita 3**
   **Kimo – mita 1**
3. Njia itakayotumika **MOROGORO hadi NAMANGA kupitia CHALINZE ROAD** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115236102


# JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO,
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SAMATTA AFUZU KUCHEZA LIGI YA MABINGWA ULAYA

Ni baada ya klabu yake kutwaa ubingwa wa Ubelgiji msimu huu...

**BRUSSELS, Ubelgiji**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, ameisaidia klabu yake, KRC Genk kutwaa taji la Ligi Daraja la Kwanza A nchini Ubelgiji baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya wenyeji, Anderlecht katika mechi iliyochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Constant Vanden Stock jijini Brussels.

Kwa sare hiyo, Genk imefikisha pointi 51 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote kuelekea mechi za mwisho za msimu, baada ya wapinzani wao wa karibu, Club Brugge kufungwa mabao 2-0 na Standard Liège hivyo kubaki na pointi zao 47.

Katika mchezo huo, Genk walitangulia kwa bao la kiungo Mbelgiji, Bryan Heynen dakika ya 11, kabla ya mshambuliaji Mkongomani na mzaliwa wa Ufaransa, Yannick Bolasie kuisawazishia Anderlecht dakika ya 65.

Pamoja na kuipa ubingwa wa Genk, lakini Samatta ambaye alipumzishwa kipindi cha pili nafasi yake ikichukuliwa na kiungo Mbelgiji, Casper De Norre, pia anaiwezesha timu yake kukata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Na baada ya mchezo huo, kikosi cha Genk kimerejea nyumbani mjini Genk kwa furaha ambako leo kutakuwa na sherehe za ubingwa.

Samatta ambaye hapa nchini alichezea African Lyon na Simba zote za jijini Dar es Salaam, pia amefanikiwa kuwa mfungaji bora wa Ligi hiyo ya kimataifa maarufu Jupiler kwa kupachika wavuni mabao 23 msimu huu.

Kwa ujumla, Samatta mwenye umri wa miaka 26, ameifungia Genk mabao 62 katika mechi 155 za mashindano yote tangu amejiunga na timu hiyo Januari mwaka 2016 akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Katika ligi ya Ubelgiji pekee amefunga mabao 47 katika mechi 122, kwenye Kombe la Ubelgiji amefunga mabao mawili katika mechi tisa na Ligi ya Europa amefunga magoli 14 katika mechi 24 zilizoshuka dimbani kwenye michuano hiyo.

## KWA UFUPI

### SALAH ATAKIWA MADRID
REAL Madrid inajiandaa kufanya jaribio la kutuma ofa kwa Liverpool ili kumsajili mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah (26) katika kipindi cha majira ya joto. ***(Canal+, via Mail)***

### ZIDANE AMTAKA JOVIC
MSHAMBULIAJI wa Eintracht Frankfurt na Timu ya Taifa ya Serbia, Luka Jovic (21), ambaye dau lake ni pauni milioni 52.4 yuko katika rada za Real Madrid. ***(Sky Sports)***

### GRIEZMANN SOKONI RASMI
BARCELONA inajipanga kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Antoine Griezmann, ambaye tayari ameshatangaza kuondoka Atletico Madrid. ***(Goal.com)***

### GRIEZMANN ATAJWA CITY
MABINGWA wa Ligi Kuu England, Manchester City, wako tayari kutoa dau litakalotajwa ili kumnasa straika Mfaransa Antoine Griezmann, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Sport, via Manchester Evening News)***

### LEWANDOWSKI ANUKIA UTD
MANCHESTER United, imeweka wazi nia yake ya kumsajili straika wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski (30), ambaye tayari amesema hataki kusajili mkataba mpya na klabu hiyo ya Ujerumani baada ya mkataba wake wa sasa kumalizika ifikapo 2021. ***(Kicker, via Express)***

### UNITED YAMWANIA DEMBELE
MSHAMBULIAJI wa Lyon mwenye umri wa miaka 22 ambaye pia yuko katika kikosi cha Timu ya Vijana ya Ufaransa, Moussa Dembele, naye ametajwa kuwaniwa na Manchester United ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 40. ***(Sun)***

### RICHARLISON KUIKAMUA PSG
EVERTON itahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 65 kutoka kwa Paris St-Germain kama mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa watamtaka mshambuliaji wake Mbrazil Richarlison ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Star)***

### ALEXIS KUKUBALI HASARA
WAKALA wa mshambuliaji wa Manchester United, Alexis Sanchez (30), anatarajia kufanya mazungumzo na klabu za Juventus pamoja na Inter Milan ili kuangalia uwezekano wa nyota huyo wa Chile kukubali kushiriki sehemu ya kupunguza dau lake kwa lengo la kurahisisha mchakato wa kuondoka Old Trafford. ***(Corriere dello Sport, via Metro)***

### DYBALA : NAONDOKA JUVE
WAKALA wa mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala amesema kuwa mchezaji huyo ataondoka katika klabu hiyo ya Italia, tayari Atletico Madrid na Manchester United zimeonyesha nia ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Mirror)***

### ATLETICO YAMFUATA ALONSO
BEKI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Hispania, Marcos Alonso, ambaye ana umri wa miaka 28 anawindwa na Atletico Madrid katika kipindi cha usajili cha majira ya joto. ***(AS - in Spanish)***

### BRANDT KUBAKIA BAYERN
MSHAMBULIAJI wa Bayer Leverkusen Mjerumani, Julian Brandt (23), anajiandaa kukacha ofa kutoka Tottenham na Liverpool kwa lengo la kubakia kwenye klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Sky Germany, via Mirror)***

### CAKIR KUTUA LIVERPOOL
LIVERPOOL imeanza mawasiliano na Trabzonspor kwa ajili ya kumwania mlinda mlango wa klabu hiyo ya Uturuki, Ugurcan Cakir ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Express)***

### BARCA YAMFUATA AUBAMEYANG
BARCELONA imetangaza nia ya kumsajili mshambuliaji wa England na Manchester United, Marcus Rashford (21), pamoja na mastraika wawili wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang (29) , ambaye ni raia wa Gabon na Mfaransa Alexandre Lacazette. ***(Mundo Deportivo)***

## HABARI MICHEZO

# KASEJA APIGIWA CHAPUO KUONGEZWA STARS AFCON

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Ettienne Ndayiragije, amesema kuwa kipa mkongwe nchini, Juma Kaseja, anapaswa kuwapo katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars) kitakachoelekea katika Fainali za Kombe la Afrika (AFCON 2019) ambazo zitafanyika kuanzia Juni 21 hadi Julai 13 mwaka huu nchini Misri.

Taifa Stars imepangwa katika Kundi C pamoja na vigogo Algeria, Senegal na majirani zao Kenya maarufu Harambee Stars.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ndayiragije, alisema kuwa Kaseja anahitajika katika kikosi hicho kutokana na uzoefu alionkuwanao ambao anaweza kuwasaidia makipa na wachezaji wake na si lazima kucheza.

Ndayiragije alisema kuwa anaamini kipa huyo wa zamani wa Simba na Yanga akijumuishwa katika msafara wa timu hiyo, atasaidia kuwaongezea ujuzi wachezaji walioko kwenye kikosi hicho na Taifa Stars inaweza kufanya vema katika fainali hizo.

"Ninaamini Kaseja anastahili kuwamo katika kikosi cha Taifa Stars, sio lazima awe mchezaji, lakini uwepo wake ni muhimu katika afya ya timu, ana vitu vingi vya kiufundi ambavyo vitakuwa ni msaada mkubwa kwa wachezaji wenzake, hayo ni maoni yangu," alisema Ndayiragije.

Aliongeza kuwa baada ya Taifa Stars kufuzu, sasa inatakiwa kutumia nguvu zaidi kukiandaa kikosi chake ili kiweze kushindana na hatimaye kufika mbali kwenye michuano hiyo.

"Sasa wanatakiwa waangalie walitumia nguvu gani wakati wanataka kufuzu, na wajipange vipi ili kwenda huko wakiwa imara, ni wakati wa viongozi kujiuliza na kutekeleza vema mipango yao, naamini wakiwa imara watafika mbali kwa sababu mechi za michuano hiyo ni chache kama vile wanavyoenda katika mashindano ya CECAFA," aliongeza kocha huyo.

Stars ambayo iko chini ya Mnigeria Emmanuel Amunike imefuzu fainali hizo baada ya kuzikosa kwa miaka 39 na ni baada ya kumaliza wakiwa wa pili kwenye Kundi L ambalo liliongozwa na Uganda (The Cranes).

Katika kujiandaa na fainali hizo, tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) limesema kuwa Stars itacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Misri ifikapo Juni 13 jijini Cairo.



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kushoto) akijiandaa kumtoka beki wa Mtibwa Sugar, Cassian Ponera katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 3-0. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

## Geita Gold FC waanza vizuri

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya kwanza hatua ya mtoano dhidi ya JKT Mlale iliyochezwa juzi, Chama cha Soka cha Mkoa wa Geita (GEREFA), kimesema kuwa timu yao bado ina "safari" ndefu ya kuwania kupanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mechi ya marudiano kati ya JKT Mlale dhidi ya Geita Gold FC itachezwa Mei 22 mwaka huu kwenye Uwanja wa Majimaji Mjini Songea.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa GEREFA, Pius Kimishi, alisema kuwa timu yao inahitaji kupambana kwa kiwango cha juu ili iweze kutimiza ndoto zake za kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kimisha alisema kuwa anawaomba wadau na mashabiki wa soka wa Geita kushirikiana na uongozi wa timu hiyo ili waweze kufanya vema na hatimaye ndoto zao za kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kutimia.

**"Bado tuna safari ndefu, tumeshinda, tunahitaji kulinda matokeo yetu, na tukifanikiwa kusonga mbele, tutasubiri kucheza mechi nyingine mbili na timu ya Ligi Kuu ambayo itakuwa iko kwenye hati hati ya kushuka daraja, huu mfumo ni mgumu la kini unaongeza ushindani katika ligi zote," alisema Kimisha.**

Tayari Polisi Tanzania imeshapanda daraja kutoka Kundi B sambamba na Namungo FC ya Lindi huku African Lyon yenyewe imeshuka daraja kutokana na kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

# SportPesa imeleta msisimko wa soka

**Na Mwandishi Wetu**

KIPINDI cha mwaka 1990 hadi 2000, vituo vya redio na televisheni ndio vilikuwa vyanzo pekee vya kuniweka karibu zaidi na msisimko halisi wa soka.

Miaka hiyo ukisikia majina kama Nteze John 'Rungu', Ally Mayay 'Tembele', Juma Kaseja basi bila shaka unajua wababe wa nchi wanafanya yao kwenye Uwanja wa Uhuru kipindi hicho ukijulikana kama 'Shamba la Bibi'.

Simba dhidi ya Enyimba, Yanga dhidi ya Zamalek ndio zilikuwa mechi kubwa ambazo ukimsikia Juma Nkamia akitangaza pande za RTD basi ni lazima uongeze umakini usipitwe hata na nukta.

Shauku inarudi tena

Kwa shabiki ambaye amezoea kwenda uwanjani kuiona Simba au Yanga ikicheza mara kwa mara dhidi ya timu za Tanzania au kutoka nchi nyingine za bara la Afrika, huwa na shauku ya kawaida tofauti na yule ambaye ni mara yake ya kwanza.

Leo hii tunazungumzia timu kama Sevilla kutoka nchini Hispania kuja Tanzania kucheza dhidi ya Simba kwenye dimba la Taifa.

Hii ni mechi kubwa ambayo hata kama umeshaitazama Simba Uwanjani mara 1000 basi bila shaka ungetamani kuwepo kuona jinsi wababe hao wa LaLiga wakisakata kabumbu la kihispaniola kwenye ardhi yetu.

Sevilla inakuwa ni timu ya pili kubwa kutoka barani Ulaya kutembelea Tanzania na kucheza mechi ya kirafiki baada ya Everton kufanya hivyo mwaka 2017 chini ya udhamini wa kampuni ya michezo ya kubashiri ya SportPesa.

Tunaizungumzia Sevilla iliyotwaa ubingwa wa Europa League mara tatu mfululizo chini ya Unai Emery.

Unapozungumzia Sevilla kuja Tanzania kucheza na bingwa wa nchi, ni zaidi ya mechi ya Simba na TP Mazembe au Al Ahly kwa sababu hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa bingwa wetu kuumana na klabu kutoka LaLiga kwenye ardhi yetu ya nyumbani.

Uso kwa uso

Tusubiri kuiona hiyo vuta ni kuvute ya mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara, Meddie Kagere dhidi ya beki shupavu kama Simon Kjaer ambae almanusura aipeleke timu yake ya taifa ya Denmark kwenye nusu fainali ya Kombe la dunia nchini Urusi huku James Kotei na Jonas Mkude watakavyomdhibiti Pablo Sarabia ambaye amepika mabao 17 mpaka sasa kwenye msimu huu.

Tusubiri kuona jinsi Mohamed Hussein na Zana Coulibaly watakavyowazuia mawinga wasumbufu wa Sevilla kama vile Jesus Navas na Quincy Promes.

Pia tusubiri kuona jinsi beki mkongwe, Erasto Nyoni atakavyotoana jasho na mshambuliaji hatari kama Wissan Ben Yedder ambaye ameifungia Sevilla mabao 29 kwenye mashindano yote msimu huu hadi sasa.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. SIMBA | 34 | 27 | 4 | 3 | 72 | 14 | 85 |
| 2.YANGA | 36 | 26 | 5 | 5 | 55 | 25 | 83 |
| 3. AZAM | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. KINONDONI MC | 36 | 11 | 16 | 9 | 36 | 25 | 49 |
| 5. MTIBWA SUGAR | 36 | 14 | 7 | 15 | 36 | 32 | 49 |
| 6. LIPULI | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7. NDANDA | 36 | 12 | 11 | 12 | 23 | 31 | 47 |
| 8. MBEYA CITY | 35 | 13 | 7 | 15 | 36 | 36 | 46 |
| 9.SINGIDA UNITED | 36 | 11 | 12 | 13 | 28 | 35 | 45 |
| 10. STAND UNITED | 36 | 11 | 8 | 16 | 36 | 48 | 44 |
| 11. ALLIANCE | 36 | 11 | 11 | 14 | 29 | 38 | 44 |
| 12. COASTAL UNION | 36 | 10 | 14 | 12 | 31 | 42 | 44 |
| 13. MBAO | 36 | 11 | 11 | 14 | 26 | 38 | 44 |
| 14. TANZANIA PRISONS | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 15. KAGERA SUGAR | 36 | 10 | 13 | 13 | 32 | 40 | 43 |
| 16. RUVU SHOOTING | 36 | 10 | 12 | 14 | 35 | 48 | 42 |
| 17. JKT TANZANIA | 36 | 9 | 14 | 13 | 22 | 32 | 41 |
| 18. BIASHARA UNITED | 35 | 10 | 10 | 15 | 26 | 32 | 40 |
| 19. MWADUI | 36 | 10 | 8 | 18 | 38 | 48 | 38 |
| 20. AFRICAN LYON | 35 | 4 | 10 | 21 | 21 | 47 | 22 |

# Michezo

Jumamosi Mei 18, 2019

Nipashe




**Samatta afuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya**

HABARI UK 30

# AUSSEMS: TUMEUKARIBIA UBINGWA

## ●●●Lakini Mbelgiji huyo asema wanahitaji kushinda mechi zote zilizobakia...

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi, Patrick Aussems, amesema kuwa ushindi walioupata katika mchezo wa juzi dhidi ya Mtibwa Sugar umewafanya kuukaribia ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Simba ilirejea katika mbio hizo za ubingwa baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 kutoka kwa Mtibwa Sugar na kukaa katika uongozi wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems alisema kuwa anashukuru na anawapongeza wachezaji wake kwa kupata ushindi katika mchezo huo ambao ulikuwa na ushindani kutokana na wapinzani wao kujipanga kuondoka na ushindi pia. Aussems alisema kuwa wanaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha wanapata ushindi mwingine katika mechi dhidi ya Ndanda FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**"Uchezaji makini mzuri, soka bora na kutumia nafasi vema, lakini tulikuwa makini katika kiwango cha juu katika dakika 20 za mwisho, ni moja ya vitu vilivyotusaidia kupata ushindi, lakini kitu muhimu ni kuwa tumekaribia kufikia malengo yetu," alisema Aussems.**

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa wanaendelea kuwashukuru mashabiki wa timu hiyo na wanaahidi kupambana ili kuwapa matokeo yatakayowafurahisha.

Naye mshambuliaji wa kimataifa wa timu hiyo Mganda Emmanuel Okwi, alisema kuwa wamejiandaa kuendelea kupambana ili kupata ushindi katika mechi yao inayofuata dhidi ya Ndanda FC kwa sababu wanahitaji kutetea taji la ubingwa wa Bara ambalo wanalishikilia.

"Pointi zimetusogeza mahali pazuri kuelekea katika mbio za ubingwa, kuteleza ni sehemu ya mchezo, tuliteleza mechi mbili zilizopita," alisema Okwi.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema kuwa wamekubaliana na matokeo hayo ambayo yametokana na mbinu walizoingia nazo uwanjani kushindwa kufanya kazi.

"Tulijiandaa kupata pointi tatu katika mechi hii, lakini mipango yetu haikufanya kazi, tunaendelea kujipanga ili kurejea tukiwa imara katika mechi zilizosalia," alisema kocha na mchezaji wa zamani wa timu hiyo.

Mtibwa Sugar itaikaribisha Simba katika mechi ya mwisho msimu huu itakayochezwa Mei 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro wakati Yanga itakuwa kwenye Uwanja wa Uhuru kuvaana na Azam FC.



Mshambuliaji wa mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City, Sergio Aguero, akiwa katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kuivaa Watford katika mechi ya fainali ya Kombe la FA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Wembley. **PICHA: MTANDAO**

## Ndayiragije aamua kumfunda kocha Zahera

**Na Mwandishi Wetu**

KILA mtu afanye kazi yake. Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa KMC FC ya Kinondoni jijini Dar es Salaam ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Etienne Ndayiragije kuhusiana na viwango vya waamuzi wanaochezesha ligi hiyo hapa nchini.

Akizungumza katika mahojiano maalumu na gazeti hili jijini, Ndayiragije, alisema kuwa anashangazwa kumuona Kocha Mkuu wa Yanga Mkongomani Mwinyi Zahera akilalamika kila mara kuhusiana na waamuzi jambo ambalo kitaaluma si sahihi. Ndayiragije alisema kuwa ifike wakati kila mmoja akafanya kazi yake na kuacha tabia ya kuingilia majukumu ya watu wengine kwa malengo ya kujilindia heshima.

"Kila mtu afanye kazi yake, mimi siwezi kuzungumzia waamuzi kwa sababu si kazi yangu, mimi ni kocha, hiyo ni kazi ya msemaji wa timu, ndio maana kila klabu imeajiri wafanyakazi tofauti," alisema kocha huyo wa zamani wa Mbao FC ya jijini Mwanza. Ndayiragije aliongeza kuwa anafurahi kuona hadi sasa timu yake imefikia malengo ya kubakia kwenye ligi hiyo, lakini anaamini akiendelea kubaki katika kikosi hicho atahakikisha inatwaa ubingwa wa Bara.

"Tunatakiwa tujipange kuhakikisha siku moja KMC inakuwa kama Simba, Yanga au Azam, hata hizi zilianza kama KMC, tutengeze timu na tuwe na maandalizi bora, tutafika huko, lakini sio kazi ya muda mfupi, inahitaji muda na uwekezaji wa kutosha," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Hata hivyo Ndayiragije ameendelea kukataa kufunguka kuhusu hatima yake baada ya kuwapo kwa fununu za kutakiwa na kikosi cha mabingwa wa Kombe la Kagame, Azam FC.

Kocha huyo anatarajia kumaliza mkataba wake wa kuifundisha KMC baada ya kumalizika kwa msimu huu, na baada ya hapo atakuwa huru kufanya mazungumzo na klabu yoyote inayohitaji huduma yake kutoka ndani au nje ya Tanzania.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, amesema kuwa klabu yake bado inamtambua mshambuliaji, Heritier Makambo kuwa ni mchezaji wake halali na alipata ruhusa ya kuondoka nchini kwenda Horoya FC kufanya vipimo vya afya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002